# Nipashe

Jumamosi Machi 21, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580185

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Kikongwe abakwa hadi kufa, akatwa sikio, nyayo na vidole

UKURASA 4




UKURASA 13

TISHIO CORONA

# Upinzani wataka mipaka ifungwe

**WATAKA** wanaoingia wawekwe karantini, Zitto ashauri mfumo rasmi utoaji taarifa, TEC yatoa mwongozo wa ibada, Jafo awabana ma-DC wanafunzi kuzagaa stendi...*Endelea ukurasa 2, 3, 8, 10, 11, 12*



Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akizungumza kabla ya kuanza kwa ibada maalum ya maombi ya kiimani kuomba Mwenyezi Mungu aliepushe taifa na ongezeko la wagonjwa wa virusi vya Corona nchini, iliyofanyika wilayani humo, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## DC Sabaya aagiza msako walanguzi 'mask', majitiba

UKURASA 2



## BAA LA CORONA

VIRUSI vya corona bado ni tishio duniani. Taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) na machapisho mbalimbali ya wataalamu wa afya yanabainisha kuwa matumizi ya rimoti za televisheni, kingo za ngazi za maghorofa, vitufe vya lifti za maghorofa na ATM, vipaza sauti, kompyuta na simu yanaweza kusambaza virusi vya corona ikiwa vifaa hivyo vinatumiwa na watu wengi.

## DEREVA AFARIKI NDANI YA BASI

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


MICHEZO **USAJILI YANGA GUMZO JIPYA** UK. 32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# DC Sabaya atangaza msako wanaopandisha bei 'sanitizer'

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKATI Tanzania ikiwa imefikisha idadi ya watu sita waliogunduliwa kuugua virusi vya corona, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ameamuru kukamatwa wafanyabiashara na kufungwa maduka yote ambayo yatabainika kupandisha bei ya barakoa na maji dawa.

Ameagiza kuanza mara moja kwa ukaguzi wa dharura katika maduka yanayouza vifaa vya kujikinga na maambukizi ya homa hiyo kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona.

Ole Sabaya aliagiza kuanza kwa msako huo jana mchana, wakati akizungumza na viongozi wa dini kabla ya kuanza ibada maalum ya kumwomba Mwenyezi Mungu aliepushe taifa na janga la corona ambalo sasa ni janga la dunia.

"Sisi kama serikali tutachukua hatua za kibinadamu lakini kazi ya kukomesha au kuondoa hii corona katika nchi ni kazi ya Mungu mwenyewe ndio maana tuko hapa leo. Tulikuwa tunanunua 'sanitizer' (maji dawa) kwa Sh. 2,500, leo hii watu hapa wanauza Sh. 10,000 hadi 15,000 kwa pea moja. Tulikuwa tunanunua spiriti ambayo ilipaswa kuuzwa kwa Sh. 10,000 lakini sasa inauzwa Sh. 20,000 mpaka Sh. 25,000.

"Watu walikuwa wananua mask (barakoa) za kawaida mitaani Sh. 1,000 mpaka 2,000 leo inauzwa Sh. 10,000 mpaka 15,000. Ibilisi naye ameingia kazini. Nimeelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai awaagize maofisa biashara wote leo (jana) kupita maduka yote.

"Tukikuta uthibitisho wowote kama umetumia nafasi hii ya watu wanaoteseka ya watu wanaotaabika, wanaoumwa katika wakati ambao taifa liko katika hakikisho la usalama wa kila mtu umepandisha bei, hatua ya kwanza ni kufunga hilo duka lako na tukija kukurejeshea tukimaliza tunakuja kukuuliza ilikuwaje utese watu wa Mungu, na hayo maduka mkurugenzi yatafungwa leo (jana)," alisema.

Kuatika ibada hiyo, Sabaya aliwataka viongozi wa dini wawe na imani kwamba nchi itaponywa kupitia maombi yao kwa kuwa nchi iko katika taharuki, dunia iko katika taharuki, matajiri wa dunia uchumi wao tayari umeshatikiswa, viranja na manyapara wote duniani wanahangaika jambo moja ambalo ni corona.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Aidha, Ole Sabaya alisema moja ya mambo watakayoyafanya ni kujitahidi kwamba angalau katika kipindi hiki cha ugonjwa, Mungu aendelee kuwapa neema watu wasitindikiwe na kitu kwa kudhulumiwa kupitia ugonjwa huu.

Alisema ofisi yake itahakikisha hakuna anayedhulumiwa wala anayeonewa na kwamba hivi sasa wafanyabiashara na maofisa biashara watakwenda kuhakikisha kwamba yale ya kibinadamu kama upandishaji wa bei holela na dhuluma inayofanyika kwa makusudi inakomeshwa na watu hao kuchukuliwa hatua.

"Kamwe hatutakubali kwamba kitu wanajua kinauzwa Sh. 2,000 halafu kinauzwa 20,000, hilo halitasubiri maombi ya Mungu litasubiri sisi tufanye kazi tuchukue hatua.

Tumechagua leo (jana) kwa sababu katika nchi kama ambavyo viongozi wa dini mmetueleza iko 'tauni' aina ya corona ambayo imevamia nchi na uwezo wa kibinadamu wa kawaida unaonekana umeshindwa. Ulaya wanahangaika kwa njia zao zote, wamekosa suluhu ndio maana Asia wanahangaika kwa njia zao zote wamekosa suluhu na majibu," alisema.



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Simon Sirro, akinawa mikono kabla ya kuingia ofisini kwake, katika Makao Makuu ya Jeshi hilo, jijini Dodoma jana, ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (COVID –19). **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Upinzani wataka mipaka ifungwe

**Na Mary Geofrey**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, umeitaka serikali kufunga mipaka yote ya nchi ili kukabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

Cecilia Paresso, Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, aliyasema hayo jana jijini Dodoma.

Waziri Kivuli huyo pia aliitaka serikali kuhakikisha watu wanaoingia nchini kutoka nje ya nchi, wawekwe chini ya uangalizi maalum kwa siku 14 kwa gharama zao ili kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo.

"Bila shaka sote tunatambua nchi yetu imekubwa na janga la mlipuko wa ugonjwa wa Corona ambao unaletwa na virusi vya COVID19.

"Kwa kutambua umuhimu wa uhusiano wa afya na nguvukazi ya taifa, sisi kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka serikali pamoja na mambo mengine kusimamia udhibiti wa janga hili kwa umakini na weledi mkubwa," alisema.

Paresso alisema hatua ya kufunga mipaka na kuwaweka karantini wageni wanaotoka nje ya nchini ni kutokana na kuwa wagonjwa walipo nchini ni wale waotoka nchi mbalimbali duniani.

"Tunatambua athari za kufunga mipaka ya nchi katika wakati huu wa utandawazi wa kibiashara na kiuchumi. Hata hivyo, afya na uhai wa mwanadamu haiwezi kulinganishwa na thamani ya kitu chochote.

"Ni vema kwa sasa tusiangalie na kuwaza tu faida za muda mfupi katika za utalii, biashara na uchumi kwa kuacha mipaka wazi jambo ambalo litakuja kutufanya tujute baadaye kama taifa," alisisitiza.

Aliitaja serikali kuwaweka chini ya uangalizi maalum kwa siku 14 watu wanaoshukiwa kuwa na maambukizi ili kubaini kama wana maambukizo au la badala ya watu kutangazwa ndani ya muda mfupi kama ilivyo sasa.

Alitolea mfano, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliyetangaza kuwa dereva aliyemwendesha Mtanzania wa kwanza aliyegundulika na virusi vya Corona, hana maambukizo yoyote wakati siku 14 hazijatimia tangu awekwe chini ya uangalizi.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka serikali na viongozi waliopo madarakani kutoleta mzaha kwenye swala hili na pengine ikawa bora zaidi kuwaachia wasemaji kutolea taarifa suala hili kuliko hivi tunavyoona mkanganyiko wa matamko kutoka kwa kila mtu," alisema.

Paresso aliitaka serikali ifanye jitihada za lazima kuhakikisha kunakuwapo na maabara ya kupima sampuli za virusi katika hospitali za mikoa badala ya kutumia maabara moja ya jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali pia ina jukumu la kuhakikisha usalama wa watoa huduma katika maeneo yenye mlipuko kwa kupatiwa vifaa maalum vya kujikinga na maambukizo ya virusi hivyo.

Aliitaka serikali kuhakikisha inatoa msaada wa ziada katika vituo vya kulelea watoto yatima, vituo vya wazee na vituo vya vijana walioathirika kwa dawa za kulevya kwa kuwapatia vitakasa mikono (sanitizers) na mahitaji mengine ya msingi kwa ajili ya kujilinda dhidi ya virusi vya Corona.

Paresso pia aliitaka serikali ieleze hatua inazochukua kwa ajili ya kukabiliana na athari za kiuchumi na kibiashara zitakazotokana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Alisema serikali inapaswa pia kueleza kwa kina kuhusu mikakati iliyopo ya kudhibiti msongamano katika masoko, stendi za mabasi na maduka makubwa (mall), mahabusi za polisi, magereza, makanisa na maeneo yote yenye misongamano ya namna hiyo.

"Kupitia taarifa kwenye vyombo vya habari, tumeona katazo la wageni magerezani, tunapenda kufahamu kuna mikakati gani kwa mahubusi na wafungwa wapya wanaoingia magerezani ili kutokupeleka maambukizo?" alihoji.

Alisema serikali inapaswa kutoa taarifa ya mkakati wake wa kuhakikisha kuna hifadhi kubwa ya chakula ili kuondoa upungufu unaoweza kujitokeza kutokana na mlipuko huo wa Corona hasa kwa hofu ya watu ambayo inaweza kusababisha kushuka kwa shughuli za kiuchumi na mwingiliano wa kibiashara hivyo pia kuathiri kipato cha watu.

# Latra yaongoza vyombo usafiri kuweka dawa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), imewataka wamiliki wa vyombo vya usafiri, wasafirishaji, mashirika ya reli na wafanyakazi kunyunyiza dawa za kuua virusi vya corona kwenye vyombo vyao.

Kwa mujibu taarifa yao iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu, Gilliard Ngewe, kila basi liwe na dawa za kupaka mikononi ya kuua virusi ambazo zitatumika na abiria kabla ya kuingia kwenye vyombo hivyo.

"Waendesha teksi, pikipiki za magurudumu mawili na matatu wahakikishe kuwa abiria wanapanda na sawa ya kuua virusi hivyo, magari ya mizigo hayaruhusiwi kubeba abiria yoyote.

"Idadi ya abiria kwa mabasi yanayokwenda mkoa mmoja kwenda mwingine ni kulingana na idadi ya viti vivyo hivyo kwa magari yanayosafirisha abiria kutoka mijini kwenda vijijini," ilieleza.

Pia ilisema idadi ya abiria kwenye usafiri wa Mabasi Yaendanyo Haraka (BRT), daladala ziendane na ile iliyoainishwa kwenye leseni zao.



Wananchi wakipita ndani ya maji kwenye Barabara ya Mwawaza mjini Shinyanga jana, ambayo imejaa maji kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Zitto ashauri utaratibu utoaji taarifa za corona

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameitaka serikali kuweka utaratibu mzuri wa kutoa taarifa kuhusu ugonjwa wa corona.

Alitoa rai hiyo jana, akisema utaratibu huo utasaidia kuepusha taarifa za uzushi na zinazosababisha taharuki kwa kwa wananchi.

"Naomba Rais, Makamu wake au Waziri Mkuu aweke utaratibu wa kila siku kutoa taarifa kwa kuzungumza na Watanzania na kuruhusu maswali kwa waaandishi wa habari na si vizuri viongozi kujificha nyakati hizi," alisema.

Zitto pia aliitaka serikali kuchukua tahadhari kwa kununua chakula na kukitunza ili kisaidie endapo kutatokea upungufu katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa huo.

"Tumeona kwenye nchi ambazo zimepatwa na janga hili, kuna taharuki kuhusu chakula, watu wanaenda kununua chakula kwa ajili ya kuweka nyumbani.

"Hapa nchini pia kuna hali hiyo na tunaamini madhara makubwa yatatokea kwa watu wenye hali ya chini na bahati mbaya sana akiba ya chakula kwenye ghala la chakula la taifa ni tani 42,000 za nafaka ambazo zinamtosheleza Mtanzania kwa siku mbili au tatu. "Ni vyema serikali kuchukua uamuzi wa haraka kwa kutumia fedha za mfuko wa dharula kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, kununua chakula cha kutosha na kukiweka kwenye akiba ya chakula ili pale patatokea upungufu wa chakula, serikali igawe kwenye uhitaji," alishauri.

Zitto alisema kuna haja kufanyika uchambuzi wa kina wa kiuchumi kuona maeneo ambayo madhara yake yatakuwa makubwa ikiwamo sekta ya utalii ambayo inapaswa kuangaliwa kwa kina ili kulinda ajira za Watanzania.

Zitto pia aliishauri serikali kuwasaidia makundi ya watu wenye magonjwa ya sukari na moyo kuhakikisha inawalinda ili wasipate ugonjwa huo kwa sababu wao ndiyo wako kwenye hatari zaidi ya kuathirika. Alisisitiza Watanzania wote wakiwamo viongozi wa kisiasa, wanapaswa kuwa wamoja katika kipindi hiki pasipokujali itikadi zao za vyama.

"Nimeona baadhi ya wanasiasa wanachanganya siasa la janga kama hili ambalo dunia nzima inahangaika nalo, ni janga ambalo linamhusu kila mtu na haliangalii itikadi ya chama cha siasa, huu siyo wakati wa kuchanganya mambo haya na siasa," alisema.

# Wizara yakumbusha hatua za kuzingatia

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amekutana na wataalamu wa afya kujadili hali ya mwenendo wa ugonjwa wa corona nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikali cha Wizara hiyo, masuala makubwa yaliyojadiliwa na kutolewa maelekezo katika kikao hicho ni pamoja na idara husika kuyafanyia miongozo iliyotolewa kazi ili kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Maelekezo yaliyotolewa ni kuhakikisha hospitali za serikali na binafsi zinazingatie kikamilifu miongozo ya wizara kuhusu magonjwa ya mlipuko kabla ya kuhamasisha wagonjwa kwenye hospitali za rufaa za serikali.

Pia wamelekeza serikali kuendelea kutoa elimu na maelekezo sahihi kwa wananchi kuhusu jinsi ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo, dalili zake na hali halisi ya mwenendo wa ugonjwa huo nchini.

"Wananchi wanapaswa kutambua kuwa siyo kila homa na mafua ni corona, hivyo wanashauriwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na mamlaka husika," taarifa hiyo ilifafanua. Vyombo vya habari pia vimetakiwa kutumia wataalamu wa afya kutoka Wizara ya Afya na taasisi zake pamoja na ofisi za waganga wakuu wa mikoa na halmashauri ili kuhakikisha maudhui ya ugonjwa huo yanakuwa sahihi.

"Jambo la mwisho wameelekeza wananchi kupuuzia taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii zinazotolewa na baadhi ya watu wenye nia ya kupotosha hali ya ugonjwa huo nchini.

"Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea kutoa huduma ya afya kwa watu waliothibitika kuwa na ugonjwa wa corona na kudhibiti maambukizo mapya," taarifa hiyo ilisema.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi jana mchana wakati inatolewa, hakukuwa na mgonjwa mpya aliyebainika kuwa na virusi vya corona nchini baada ya juzi idadi ya wagonjwa kufika sita, ambao wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa watumishi wa sekta za afya.

## Wataja kinachokwamisha uwekezaji viwanda sukari

**Na Enock Charles**

WAWEKEZAJI wa viwanda nchini wamesema kukosekana kwa uhakika wa soko la baadhi ya bidhaa ni mojawapo ya vikwazo vinavyochea kusuasua kwa uwekezaji katika baadhi ya sekta, ikiwamo sekta ndogo ya sukari.

Akizungumza katika kikao cha wawekezaji wa viwanda na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) jijini Dar es Salaam jana, Mfanyabiashara maarufu nchini, Shubash Patel, alisema wafanyabiashara wanapowekeza katika bidhaa fulani, hutarajia kupata faida kutokana na uwekezaji huo.

Kwa kuzingatia dhana hiyo, Patel alisema bidhaa inapokuwa haina uhakika wa soko na kunakuwa hakuna uhakika wa kupatikana kwa faida, ni vigumu kuwekeza katika bidhaa hiyo.

Akitoa mfano kwa viwanda vya sukari, alisema gharama za kuwekeza katika uzalishaji wa sukari nyeupe ni kubwa kulinganishwa na uhakika wa kupatikana kwa soko na hivyo kuwa vigumu kuwekeza katika bidhaa hiyo.

"Kwa sasa hatuna 'refinery' (mtambo wa kusafishia sukari) na kuwekeza hiyo inahitaji Dola milioni 30 (Sh. bilioni 68.894) kusafisha sukari kutoka njano kuwa nyeupe kuwa sukari ya viwandani.

"Sasa, uwekezaji kama huo ni mkubwa, lakini soko halina uhakika wa kurejesha fedha yote hiyo kiasi cha Dola milioni 30," mfanyabiashara huyo alifafanua.

Katika kikao hicho, Waziri Kairuki alisema serikali itahakikisha inaweka mazingira bora kwa wawekezaji nchini ikiwamo kuweka miundombinu wezeshi kama umeme wa uhakika na ya usafirishaji ili kuwaondelea vikwazo katika uwekezaji.

"Huwezi kufanikiwa katika viwanda kama hakuna umeme wa uhakika, huwezi kufanikiwa kama hauna miundombinu mizuri ya reli kwa sababu tunafahamu katika viwanda kunazalishwa mizigo mikubwa, kwa hiyo unapokuwa na miundombinu mizuri ya reli kwanza unapunguza gharama na pia ni usafiri wa uhakika," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

APPROPRIATE TECHNOLOGY TRAINING INSTITUTE

CHUO CHA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI – MBEYA)

TANGAZO LA KUAHIRISHWA KWA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI (LBT)

Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi "Appropriate Technology Training Institute" (ATTI-MBEYA) ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kinawatangazia kuwa kimeahirisha mafunzo ya kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo ilipangwa kuanza tarehe **06/04/2020 - 13/06/2020** Chuoni Mbeya pamoja na Kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana ya ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo ilipangwa kuanza tarehe **18/05/2020 - 13/06/2020.** Kozi hizi na tarehe mpya za kuanza mafunzo kwa kila kozi zitatangazwa tena.

Chuo kinaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Kwa maelezo zaidi Wasiliana nasi
MKUU WA CHUO
CHUO CHA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVUKAZI (ATTI – MBEYA)
S.L.P 1957, MBEYA,

Simu: 025 295 7484/5; 0787 059 555; 0769 317 404; 0765 251 509
Nukushi: 025 295 7486

Barua pepe: attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com

215676402




Kijana akiwa amebeba mzigo mkubwa kichwani, kwaajili ya kujipatia kipato cha siku, katika Mtaa wa Mkunguni, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Kikongwe abakwa hadi kufa, akatwa viungo nyeti mwilini

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

KIKONGWE anayekadiriwa kuwa na zaidi ya miaka 80, mkazi wa Kijiji cha Shaurimoyo wilayani Babati, amebainika kubakwa na kuuawa na hatimaye kukatwa vidole na watu waliomfanyia unyama huo.

Kikongwe huyo alikutwa amekufa Machi 8, 2020 baada ya kufanyiwa ukatili na watu wasiojulikana.

Mashuhuda wa tukio hilo wamesema kikongwe huyo alikutwa amekatwa vidole na kitu chenye ncha kali na kubakwa hali ambayo inaelezewa kuwa huenda ilisababisha kupoteza maisha.

Bibi huyo (jina linahifadhiwa) pia alikutwa akiwa amekatwa sehemu ya unyayo jambo ambalo limehusishwa na imani za kishirikina.

Majirani wa bibi huyo aliyekuwa akiishi peke yake, walisema mwili wake pia ulikutwa ukiwa umekatwa sikio na vidole vya mkono.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Shaurimoyo, Dismas Dodo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema baada ya kupata taarifa kutoka kwa wanakijiji, alichukua hatua ya haraka ya kuwasiliana na Jeshi la Polisi Kituo Kdogo cha Magugu.

Diwani wa Kisangaji, Adamu Ipingika, akiwa kwenye msiba wa kikongwe huyo juzi, alikemea kitendo hicho na kuwataka wanakijiji kutoa ushirikiano kwa polisi ili watuhumiwa waliofanya uhalifu huo wakamatwe na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kisangaji, John Jacob, alisema katika mwezi huu, mtoto wa miaka minne alibakwa katika kijiji hicho na mtuhumiwa mwenye miaka 30 lakini alikamatwa na kufikishwa katika Kituo Kidogo cha Polisi Magugu.

Serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakikemea vitendo vya ukatili na kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za vitendo hivyo, lakini bado matukio hayo yanaendelea kuripotiwa mara kwa mara katika Mkoa wa Manyara na maeneo mengine nchini.

Erick Luwongo, mwanasheria kutoka shirika la kutetea haki za binadamu la Haki Madini lenye makao yake makuu mkoani Arusha, alisema shirika wanaendelea kutoa elimu kwa jamii na kukemea vitendo hivyo viovu.

Alisema suala la ubakaji ni kosa la jinai na adhabu yake haipungui miaka 30 kwa mujibu wa sheria za Tanzania na kwamba ubakaji si njia sahihi ya mtu kumaliza haja zake.

Aliitaka jamii kushirikiana katika kuwabaini wahalifu wa matukio ya ukatili wa aina zote ili vyombo vinavyohusika vichukue hatua zinazostahili.

## Dereva afariki ndani ya basi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DEREVA wa basi la Isamilo lenye namba za usajili T CQB 609, Sebastian Mathias (45), amefariki dunia akiwa ndani ya basi hilo.

Tukio hilo lilitokea jana wakati basi hilo lilipofika eneo la Tinde wilayani Shinyanga likitoka Mbeya kwenda jijini Mwanza.

Ilidaiwa kuwa baada ya basi hilo kufika eneo hilo, wenzake walimshusha na kumpeleka kwenye Kituo cha Afya Tinde na alipopimwa na daktari, alibainika alikuwa ameshafariki dunia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Deborah Magiligimba, dereva huyo tangu anatoka Mwanza kwenda Mbeya, alikuwa akijisikia vibaya na wakati wa kurudi Mwanza kutoka Mbeya, walipofika Singida ikabidi abadilishane na dereva mwezake.

"Dereva huyo tangu anatoka Mwanza kwenda Mbeya alikuwa akidai kujisikia vibaya na wakati wa kurudi kutoka Mbeya kwenda Mwanza walipofika Singida ikabidi abadilishane na dereva wa pili na walipofika Tinde ikabidi wenzake wamshushe kwenye kituo cha afya Tinde na alipopimwa alikuwa tayari ameshafariki dunia," aliongeza.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti katika kituo hicho cha afya na abiria waliokuwa kwenye basi hilo waliruhusiwa kuendelea na safari yao kwenda jijini Mwanza.

# Binti adaiwa kutoa mimba gesti

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MSICHANA mwenye umri wa miaka 18, Rehema Fabian, Mfanyakazi wa mgahawa ulioko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na mkazi wa Mlali mkoani Morogoro, amedaiwa kutoa mimba ya kichanga cha kiume.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Amani katika Manispaa ya Morogoro, Ramadhani Manyanga, alisema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii kuhusiana na binti huyo kufanya kitendo hicho katika chumba alichokodi katika nyumba ya wageni iliyopo mtaa huo.

Inadaiwa kuwa binti huyo alitoa mimba ya mtoto anayekadiriwa kuwa na umri wa miezi saba tumboni juzi majira ya saa 3:00 asubuhi.

Alisema mmiliki wa nyumba hiyo, Elizabeth Mapunda, alimfuata na kumweleza kulikuwa na tukio la mpangaji wake kukaa siku mbili bila kuwalipa wafanyakazi wake fedha za chumba, lakini akamweleza kuhusu tukio la ajabu walilobaini kwenye chumba alichokodi binti huyo.

"Alisema ni kitendo cha kusikitisha na kweli nilipoingia nikashuhudia binti akilia na kila nilipokuwa nikimhoji alishindwa kujieleza. Nikamuuliza kama ametokea Mlali imekuwaje aje afanyie hiki kitendo hapa, akawa analia tu.

"Niliamua kumwambia mmiliki kuwa hilo suala ni la polisi na kwa vile kituo chetu kidogo kimefungwa, tukaamua kwenda kuripoti kituo kikuu" alisema mwenyekiti huyo.

Naye mhudumu wa nyumba hiyo ya EM aliyempokea binti huyo, Ashura Juma, alidai awali alimpokea binti huyo bila kumhisi kama alikuwa mjamzito kwa kuwa tumbo lake lilikuwa la kawaida na kama ni unene aliona ni wa kawaida. Alisema alipofuika hapo alisema anataka chumba na baada ya kumpatia, aliondoka zamu jioni bila binti huyo kulipa.

"Niliporudi asubuhi kumpokea mwenzangu akasema binti hakuwa amelipia chumba, nikaenda kumgongea ili tukabidhi hesabu lakini nikasikia anaitika kwa sauti ya chini na kusema nifungue mlango. Nilipofungua nikaona anagala gala chini akiomba msaada.

"Baada ya kumhoji alisema tumbo linamuuma na kwamba huwa ana tatizo la vidonda vya tumbo. Nilimwambia anipe namba za ndugu zake tuwapigie, akasema niwaach, na kwa vile simu ilikuwa na password (nywila) nilishindwa kufanya chochote," alisema mhudumu huyo.

Mhudumu alisema hata hela ya kulipia chumba alidai iko kwenye simu na angelipa na muda huo huo mama yake mzazi alipiga akapokea na kumwelekeza kuwa yupo hapo nyumba ya wageni na anaugulia maumivu makali ya tumbo.

"Wakati nimetoka mara moja kuwaita wenzangu na kumwamsha mmiliki wa gesti, tulirudi tena kwenye kile chumba na kukuta huyo binti yuko chooni 'anapush' (anasukuma) huku anajimwagia maji huko chini (sehemu ya kizazi) ambapo tayari mtoto alishachomoza.

"Tulipatwa na taharuki na kukimbia kumwita mwenyekiti, mtoto alivyotoka akataka amwingize chooni amflash, tukamzuia asifanye hivyo. Sasa ikawa ni kilio kama kuna msiba hapa hadi mwenyekiti alipokuja tukaenda kuripoti polisi."

Alisema mtoto huyo huenda asingefariki isipokuwa kwa kitendo cha dada yule kumwagia maji ya baridi na kugala gala naye kwenye sakafu na kumsababishia ubaridi huenda ndiko kulisababisha mtoto yule kufariki dunia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alikiri kupokea taarifa ya tukio hilo na kwamba binti huyo alikutwa na dawa mbalimbali za binadamu zikiwamo alizokuwa akitumia kwa ajili ya kutoa mimba.

**Alisema mmiliki wa nyumba hiyo, Elizabeth Mapunda, alimfuata na kumweleza kulikuwa na tukio la mpangaji wake kukaa siku mbili bila kuwalipa wafanyakazi wake fedha za chumba, lakini akamweleza kuhusu tukio la ajabu walilobaini kwenye chumba alichokodi binti huyo.**


**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA TASAC**

TASAC

## TAARIFA KWA UMMA

### MKAKATI WA KUJIKINGA NA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA KORONA KWA WATOA HUDUMA KATIKA SEKTA YA USAFIRI NA USAFIRISHAJI MAJINI

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania linawaagiza watoa huduma wote katika sekta ya usafiri na usafirishaji majini kuweka mikakati ya kukabiliana na maambukizi ya virusi vya Korona.

Watoa huduma wote ikiwa ni pamoja na wamiliki wa vyombo vya usafiri na usafirishaji majini, watoa huduma za bandari, uwakala wa meli na waondoshaji wa shehena katika bandari wanaagizwa kutekeleza yafuatayo:

1. Wamiliki wa vyombo vya usafirishaji majini wanyunyizie dawa za kuua virusi katika vyombo vyao kila mwisho wa safari.
2. Wahudumu na abiria wote wanaoingia na wanaotoka katika vyombo vya usafiri majini ikiwa ni pamoja na meli, mitumbwi na vivuko wanawe mikono kwa maji tiririka na sabuni.
3. Kuzingatia idadi ya abiria wanaoruhusiwa kwenye vyombo wanaposafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine ili kuepusha msongamano.
4. Kuweka vyombo vya kunawia mikono katika ofisi za watoa huduma za bandari, uwakala wa meli, wahakiki na waondoshaji wa shehena bandari nchini.
5. Kuhakikisha tahadhari ya kujikinga na virusi vya Korona inatolewa ndani ya vyombo vya usafiri kwa kutumia redio na runinga zilizopo kwenye vyombo hivyo.

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania litasimamia utekelezaji wa maagizo haya kama sehemu ya utekelezaji wa majukumu yake ya udhibiti wa huduma za Bandari na usafiri majini, ulinzi na usalama wa usafiri majini.

**Imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania - TASAC,**
**20 Machi, 2020**

156755

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji Bara wasisahau lala salama

**AFYA** ya wachezaji na maofisa mbalimbali wanaosimamia michezo ni moja ya mambo muhimu katika maendeleo ya michezo husika sehemu yoyote hapa duniani.

Kufuatia kuwapo kwa janga la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kupitia Bodi ya Ligi Kuu nalo lilitangaza kusimamisha ligi zake zote mpaka pale hali ya maambukizi ya ugonjwa huo yatakapodhibitika au kumalizika.

Moja ya ligi iliyosimamishwa na TFF ni Ligi Kuu ambayo ndiyo ligi ya juu hapa nchini na ndio hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ligi hiyo pia ndiyo inayotoa idadi kubwa ya wachezaji wengi katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), ambayo inakabiliwa na mechi za mashindano mbalimbali, ikiwamo fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo nazo zimesimamishwa hapo hapo itakapotangazwa tena. Tamko hilo la kusimamisha ligi ambalo lilifuata mwongozo uliotolewa na serikali wa kusimamisha mikusanyiko, limetoka katika hatua ya lala salama.

Ili kurejea wakiwa imara, ni vema timu zikahakikisha zinawaandalia programu maalumu wachezaji wao kwa sababu ya kuendeleza ushindani katika mechi zilizosalia pale ligi hizo zitakapoanza tena.

Wachezaji wanatakiwa kuendelea na mazoezi binafsi kwa timu ambazo zimevunja kambi, huku wale ambao wanaendelea na mazoezi ya pamoja, kuhakikisha wanajifua ili waweze kutimiza malengo yao ya kufanya vizuri msimu huu.

Kwa kuangalia msimamo wa Ligi Kuu Bara, bado nafasi kwenye mbio za kuwania ubingwa iko wazi kutokana na timu tano zilizopo juu zinaweza kulitwaa kombe hilo endapo, vinara na mabingwa watetezi Simba watapoteza michezo yao. Klabu zinatakiwa kutumia muda huu kurekebisha upungufu waliyoubaini katika mechi zilizopita na mara watakapoanza kucheza tena, vikosi vyao kushuka dimbani wakiwa na nguvu na wanaoonyesha ushindani kuanzia dakika ya kwanza hadi ya mwisho ya mchezo husika.

Hakuna kisichowezekana na ni makosa kwa timu kukata tamaa. Timu isiyotarajiwa inaweza kutwaa ubingwa na vile vile timu isiyotarajiwa inaweza kuteremka daraja kama itazembea katika michezo yake iliyobakia kama ambavyo tunashuhudia klabu ya KMC FC ya jijini Dar es Salaam ilivyozinduka na kuanza kuvuna pointi.

Nipashe inawakumbusha wachezaji na waamuzi kuwa makini katika muda uliobakia ambao ni muhimu kwao kujiweka sokoni kuelekea maandalizi ya msimu mpya kwa kuonyesha ubora wa hali ya juu.

Tunahitaji kuona msimu ujao wachezaji wanaocheza soka la kulipwa wanaongezeka pamoja na waamuzi watakapopata beji za Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), wanakwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika mechi zote watakazopangiwa.

Haipendezi kuona kila msimu idadi ya waamuzi wanaochezesha Ligi Kuu Bara au mashindano ya Kombe la FA wanafungiwa kwa sababu ya kushindwa kumudu michezo au wachezaji wanakosa namba katika vikosi vya kwanza kufuatia kushuka viwango vyao. Kama wachezaji watautumia vema muda wa siku 30 ambao hawatacheza mechi za mashindano, watarejea na nguvu mpya na hatimaye mwisho wa msimu timu bora itatwaa ubingwa wa Bara sambamba na timu zitakazopanda daraja.

Ni wazi mchezaji atakayeonyesha kiwango bora katika mechi zilizosalia atakuwa na nafasi nzuri ya kusajiliwa na klabu nyingine kwa dau nono au kuboreshewa maslahi yake katika timu aliyopo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Michezo isifanywe uadui

**MCHEZO** ni jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Pia ni kazi ya sanaa ambayo huigizwa kwa ajili ya kuelimisha na kuburudisha watu.

Aidha ni jambo ambalo mtu hulifanya kwa kupitisha wakati au kujifurahisha; masihara.

Kwa waliofuatilia tamthilia ya 'Mambo hayo' iliyorushwa na runinga ya ITV miaka ya nyuma, nadhani wanamkumbuka Mzee Kambaulaya au baba Bishanga alipokuwa na vijana kwenye michezo ya kuigiza.

Ndiye mwandishi wa makala unayosoma sasa na kila Jumamosi kwenye gazeti hili ukurasa wa 6: 'Muungwana Lazima Nilonge.'

Nimekuwa mwanachama kindakindaki (halisi) wa Yanga tangu mwaka 1966 kwa kadi namba 447 na ya sasa ni namba 007887 (Daima mbele nyuma mwiko). Sare nne mfululizo ilizopata Yanga, baadhi ya watani (Simba) waliniita 'mzee wa sare sare!' Sikatai kwani ndio utani.

Mchezo wa kandanda abadan (katu) si vita au chuki baina ya wachezaji wala watazamaji wa pande zote zinazopambana.

Ni mchezo unaojenga ushupavu (tabia ya kuwa imara, ukakamavu) wa wachezaji na kuwafurahisha watazamaji, yaani wanachama wa timu na mashabiki wanaotoa fedha zao kuburudishwa nao.

Hakuna sababu ya kuchukiana, kuharibu vifaa vya uwanjani, kutukanana matusi ya nguoni na hata kupigana. Kwa nini watu wapigane ilhali wamekwenda kuburudika, kuona wachezaji wanavyopigana chenga, 'kuvalishana kanzu' mbwembwe zao na kufungana mabao? Hiyo ndio raha ya mchezo wa kandanda.

Nathubutu kusema kandanda ni mchezo unaopendwa zaidi duniani kuliko michezo mingine yote. Hali hiyo inathibitishwa na baadhi ya wanachama au mashabiki wa timu za Simba na Yanga wanaozirai viwanjani na pengine kupoteza maisha timu zao zinapofungwa!

Kuna mambo yanayosababisha matukio hayo. Mbali ya upenzi uliokithiri kwa timu hizi mbili nchini, pia kuna wanaowekeana madau (fedha au vitu wanavyoahidi watu kutoa kwa wanaoshindana wakati wa michezo) .

Waliokubaliana kuwekeana dau ya hela, nyumba n.k. wanapoona timu yao ina dalili ya kupoteza mchezo au tayari imepoteza, ndipo hupatwa na mshtuko na kuzirai ama kufa.

Pamoja na maafa (tukio linalosababisha madhara) hayo, kuna baadhi ya wanaojiwekea nadhiri (ahadi anayoweka mtu kwa Mwenyezi Mungu ya kufanya jambo fulani vizuri au inavyopasa iwapo atafanikiwa katika haja yake) wakisahau kuwa "Ahadi ni deni na deni ujuzie." Maana yake ahadi ni kama deni, mtu akitoa ahadi lazima aitimize. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutimiza ahadi tutoazo.

Mchezo wa kandanda una mambo matatu: Kushinda, sare au suluhu, na kushindwa. Timu inayoshinda ndio huzawadiwa kama walivyosema wahenga kuwa "Mcheza kwao hutuzwa.) Methali hii yatufunza kuwa mtu anayefanya jambo vizuri au inavyopasa hutuzwa au hupewa zawadi.

Starehe (jambo linalompa mtu raha) ya kandanda ni timu kucheza kwa nidhamu bila vurugu wala hasira. Je, Simba na Yanga zichezapo watazamaji hupara starehe?

Siku hizi ni nadra sana timu kumaliza mechi bila baadhi ya wachezaji wa timu zote mbili kuonyeshwa kadi za njano au nyekundu na kutolewa nnje ya uwanja. Kama mpira ni burudani na starehe, kwa nini wachezaji waumizwe kwa makusudi viwanjani?

Mchezaji unayemchezea mwenzako rafu, ukifanyiwa wewe utafurahi au utalipiza (kitendo cha kumfanyia jambo mtu kwa nia ya kurejesha ubaya aliofanyiwa) kisasi?

Tulimwona Rais John Magufuli alivyovaa siku Yanga ilivyoikaribisha Simba uwanja wa Taifa. Kwa kuwa Magufuli ni Rais wa Tanzania, alivaa shati lenye rangi na nembo za klabu zote mbili.

Alifanya hivyo kuonyesha kuwa timu zote ni za Tanzania hivyo zote zinamhusu. Hakutaka kuonesha anapendelea timu ipi kati ya Yanga na Simba ingawa binadamu hawakukosa la kusema. Eti kwa kuwa rangi na nembo ya Yanga ilikuwa upande wa kulia na Simba upande wa shoto tayari alionyesha msimamo wake ...!

Yanga na Simba ni timu za Mkoa wa Dar es Salaam unaoongozwa na kumilikiwa na mtu aitwaye Paul Makonda ambaye bila 'kumunyamunya', kiongozi huyo ni shabiki wa Simba.

Hakuna ubaya kwani kila mtu ana chaguo lake. Kwa kuwa timu zote mbili ni za mkoa anaousimamia, hakuwa sahihi kutamka maneno ya kejeli dhidi ya Yanga ilipofungwa bao 1-0 na timu ya Manispaa ya Kinondoni (KMC). Alisahau kuwa ofisi na makazi yake ni wilaya ya Ilala iliko Yanga?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Waziri aingilia kati mgogoro mapadri na DC

**Na Munir Shemweta,**
UKEREWE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameagiza kufanyika utambuzi wa mipaka sambamba na kuweka alama katika eneo lenye mgogoro wa ardhi kati ya Kanisa Katoliki, wananchi na Shule ya Msingi Kagunguli wilayani Ukerewe mkoani Mwanza.

Ametoa agizo hilo baada ya kuibuka mgogoro kati ya mapadri wa kanisa hilo na Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Cornel Magembe, kuhusu umiliki wa sehemu ya eneo la Shule ya Msingi Kagunguli, jambo lililosababisha mapadri kuandika waraka wa kutoshirikiana na mkuu huyo wa wilaya.

Akizungumza katika kikao cha utatuzi wa mgogoro huo uliohusisha mapadri, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Serikali ya Kijiji hicho jana wilayani Ukerewe, Dk. Mabula alisema uamuzi uliotolewa nje ya utaratibu kuhusiana na mgogoro huo ni batili na usubiriwe utambuzi wa mipaka ya eneo lenye mgogoro.

"Wizara itatuma timu ya wataalamu ili kutafuta ufumbuzi wa mgogoro kwa kubainisha na kutambua mipaka ya hapa eneo Kagunguli na kuja na ufumbuzi wa kudumu," aliahidi.

Naibu Waziri huyo pia aliagiza kupatiwa barua za maeneo yote ya taasisi za dini yenye migogoro mikubwa ya ardhi ili kushughulikiwa na kubainisha kuwa katika kuishughulikia migogoro hiyo, timu ya wataalamu itatumwa katika maeneo husika kwa lengo la kubainisha uhalali wa pande zenye migogoro.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Esther Chaula, kujiandaa kugharamia wataalamu watakaokwenda kubainisha mipaka yenye mgogoro katika halmashauri yake kwa kuwa halmashauri ndiyo zenye jukumu la kupanga maeneo yake.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, alisema kitakachofanywa na wizara yake sasa kuhusiana na mgogoro huo ni kwenda kufufua mipaka na kuainisha matumizi ya eneo hilo na kusisitiza kuwa ni vizuri maeneo yote ya umma yakawekewa mipaka yenye alama zinazoonekana.

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Magembe, aliweka wazi kuwa mgogoro ulioko katika eneo hilo umechochewa kwa kiasi kikubwa na Mkuu wa Shule ya Sekondari Kagunguli, Padri Johanes Nawachi, kwa kile anachodai padri huyo eneo la shule yake kuvamiwa.

Magembe alisema katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo, aliagiza Kanisa Katoliki kuwasilisha hati ya umiliki eneo lake, huku serikali ya kijiji nayo ikitakiwa kuwasilisha muhtasari wa kijiji kuhusiana na kutolewa sehemu ya eneo sambamba na nyumba tatu za walimu wa Shule ya Msingi Kagunguli kubaki kama zilivyo ndipo afanye uamuzi kuhusiana na mgogoro huo.

Alidai kilichofanywa na mapadri wa Kanisa Katoliki kuandika waraka wa kutoshirikiana naye ni uchochezi kwa waumini wa kanisa hilo na serikali na kubainisha kuwa hali hiyo imesababishwa na msimamo wake wa kuhakikisha maeneo ya serikali yanalindwa.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kagunguli, Padri Nawachi, alisema kumekuwa na uhusiano mbaya baina yake na Mkuu wa Wilaya Magembe baada ya kuanza kupanda miti eneo alilodai kumilikiwa na Kanisa Katoliki na kuhusisha pia maeneo ya nyumba tatu za walimu wa Shule ya Msingi Kagunguli.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko (wa pili kushoto), akikagua ufukiaji wa mabomba kwenye mradi wa maji Ziwa Victoria, Kata ya Masengwa, Wilaya ya Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 'Viwanda viboreshwe mlipuko wa Corona'

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Biashara la Afrika Mashariki, limeiomba serikali kuboresha zaidi viwanda ili bidhaa nyingine zipatikane katika viwanda hivyo hususani katika kipindi hiki cha tishio la ugonjwa wa Corona.

Akizungumza katika mahojiano na Kituo cha runinga cha ITV jana, mwakilishi kutoka baraza hilo, Raphael Maganga, alisema ni vyema viwanda vya ndani viboreshwa kwa sasa ili kusaidia pengo lililopo katika upatikanaji wa bidhaa.

"Tunanunua bidhaa nyingi kutoka China, lakini wiki iliyopita tulikuwa Kariakoo kuangalia athari zinazosababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa Corona, tulibaini kwamba upatikanaji wa bidhaa umeshuka kwa asilimia 40.

"Maana ukiangalia kuanzia Januari mpaka Februari meli nyingi hazikutoka China ambako asilimia kubwa tunachukua bidhaa hizo. Kwa hiyo, bidhaa nyingi hazijaingia Tanzania wala Afrika Mashariki, tumevikosa vitu vingi ambavyo tulikuwa tunavipata kutoka huko," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na biashara nyingi kuyumba kutokana na tishio la ugonjwa huo, wametoa mapendekezo kwa taasisi za fedha kuangalia namna ya kupunguza riba kwa wafanyabiashara wanaokopa kwa ajili ya kuendesha biashara zao.

"Katika kipindi hiki ni vyema taasisi hizi zikapunguza riba ili kusaidia wafanyabiashara kupata fedha kwa unafuu zaidi na kwa kiwango kikubwa.

"Tumependekeza kwamba kutokana na kuyumba kwa biashara nyingi, ni vyema taasisi hizi zikaangalia namna ya kusogeza muda wa kurejesha angalau miezi miwili mbele au mitatu wasilipe baadhi ya malipo ya mikopo yao angalau mpaka pale biashara zitakapoanza kurudi katika hali ya kawaida," alisema.

Alishauri kampuni za simu zinazofanya miamla ya kifedha, kupunguza gharama za makato katika kipindi hiki ambacho wafanyabiashara wengi wataitumia kufanya miamala ya kifedha ili kuepuka kuweka misongamano katika taasisi za fedha.

"Katika mapendekezo yetu, pia tumewashauri wafanyabiashara wachukue tahadhari kwa kufanya miamala ya kifedha kupitia njia za kidijitali za simu za mikononi. Na ili kufanikisha hilo, tumependekeza kampuni za simu nazo zipunguze kiwango cha makato katika kipindi hiki," alisema.

## DC awaonya Tarura madaraja kubomoka

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amewataka watendaji wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) mjini humo, kuacha tabia ya kukaa maofisi, badala yake wafanye ukaguzi wa madaraja na kuyafanyia matengenezo.

Mboneko alitoa agizo hilo juzi alipokagua daraja lililosombwa na maji katika Kijiji cha Uzogole, Kata ya Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga na barabara ya Mwawaza ambayo imeharibika kutokana na mvua na kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Alisema kwenye kipindi hiki cha mvua ni vyema watendaji wa wakala huo kuacha tabia ya kukaa maofisi, bali wafanye ukaguzi wa madaraja yote ambayo yapo katika hatari ya kusombwa na maji na kuyafanyia matengezo mapema.

"Naagiza kuanzia sasa, watendaji wote wa Tarura muache tabia ya kukaa maofisini, bali nendeni 'field' (eneo la mradi) mkague madaraja yote pamoja na barabara ambazo zimeshaharibika na kuzifanyia matengenezo, siyo kusubiri hadi zisombwe na maji na kukata mawasiliano kwa wananchi.

"Madaraja yote ambayo yamesombwa na maji pamoja na barabara zilizokatika, naagiza mzitembelee na kuzifanyia matengenezo haraka ili wananchi wapite kwa usalama na kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kutohatarisha maisha yao tena," aliagiza.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Uzogole, Peter Digo, alisema daraja kwenye kijiji hicho lina wiki moja tangu libomoke na kukata mawasiliano, huku wananchi wakilazimika kupita ndani ya maji yanayopita kwa kasi na kuhatarisha maisha yao.

Kaimu Meneja wa Tarura Manispaa ya Shinyanga, Maige Kulwa, alisema kwenye barabara ya Mwawaza, tayari wameshatenga Sh. milioni 12 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo na kuahidi kuomba fedha kwa ajili ya matengenezo ya daraja la Uzogole.

# Hakimu amwachia huru, aamuru baba akamatwe

**Na Mchael Lugendo,**
MBOGWE

MAHAKAMA ya Mwanzo Masumbwe wilayani Mbogwe mkoani Geita, imewafutia kesi washtakiwa watatu waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya wizi wa mawe yanayodhaniwa kuwa na madini ya dhahabu.

Lakini, mahakama hiyo ikaamuru kukamatwa kwa baba wa mshtakiwa wa tatu aliyefutiwa mashtaka na kuibua sintofahamu kwa wananchi waliokuwa mahakamani kufuatilia kesi hiyo.

Hakimu wa Mahakama hiyo, Godfrey Ndege, aliwafutia mashtaka Mastula Samwel, Steven Moses na Peter Jackson, waliofikishwa mahakamani hapo wakikabiliwa na kesi Na. 128/2020 ya jinai iliyotajwa kwa mara ya tatu Machi 18 na wote kukana mashtaka dhidi yao. Hakimu Ndege alisema kwa pamoja walidaiwa walitenda kosa hilo katika machimbo ya dhahabu ya Kijiji cha Nyakafulu, Kata ya Nyakafulu wilayani Mbogwe mlalamikaji akiwa ni Julius Njololo.

Kabla Hakimu Ndege hajawafutia mashtaka hayo, mshtakiwa Jackson aliomba kuwasilisha hati kutoka kwa Hakimu Mfawidhi Mahakama ya Wilaya ya Bukombe na barua ya Wakili Joannes Mbatina, akiomba kesi hiyo kuhamishiwa katika mahakama hiyo ya wilaya kutokana na mshtakiwa wa tatu (yeye mwenyewe) kupata wakili wa kumtetea. Hakimu Ndege hakuzipokea hati hizo na badala yake akatoa amri kufuta kesi hiyo kwa washtakiwa wote watatu na kuwaachia huru.

Hata hivyo, hakimu hiyo aliamuru Jackson Manyama, baba wa aliyekuwa mshtakiwa wa tatu, Jackson, kukamatwa na kisha mzee huyo na mwanawe wakasomewa mashtaka katika kesi mpya namba 143/2020 ya wizi wa kuaminiwa wa mawe yanayodhaniwa kuwa na madini aina ya dhahabu viroba 12 na Sh. 400,000, mlalamikaji akiwa ni yule yule, Julius Njololo.

Washtakiwa hao wawili waliachiwa kwa dhamana yenye masharti ya kila mmoja kuwa na mdhamini moja aliyetia saini ya bondi ya Sh. milioni 2.5 na kuwa na barua ya uthibitisho kutoka Ofisa Mtendaji wa Serikali ya Kijiji na kesi hiyo itatajwa Machi 24 mwaka huu.




Mwenyekiti wa chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), mkoani Mtwara, Saidi Swallah (kulia), akipiga makofi wakati wa uzinduzi wa Klabu ya Biashara ya NBC, mkoani humo juzi. Klabu hizo, kwa sasa zimeenea katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Singida, Morogoro, Arusha, Moshi, Mwanza, Dodoma, Njombe, Mbeya, Tanga na Lindi, ikiwa na dhumuni la kuwakutanisha, kuwaongezea ujuzi na kuwakuzia mtandao wafanyabiashara. Kushoto ni Meneja wa benki hiyo, tawi la Lindi, Ndlovin Mapunda na Meneja wa tawi la Mtwara, Emmanuel Mseti.
**PCHA: JUMANNE JUMA**

# 20 wafa kila mwaka kichaa mbwa Mara

**Na Mwandishi Wetu,**
TARIME

KATI ya watu 1,000 na 2,500 wako katika hatari ya kuambukizwa kichaa cha mbwa kila mwaka mkoani Mara huku 20 wakipoteza maisha kila mwaka kutokana na tatizo hilo.

Kutokana na baa hilo, mkakati mpya wa kutokomeza kichaa cha mbwa kwa binadamu na kuokoa maisha ya watu umezinduliwa na Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Global Health, ukilenga kudhibiti kichaa cha mbwa katika Wilaya ya Tarime.

Taasisi hiyo imeendesha mafunzo ya siku tatu kwa wenyeviti 54 wa vijiji kutoka kata 12 za wilaya hiyo ili kuwajengea uwezo kuhusu mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo na kudhibiti maambukizo mapya.

Mafunzo hayo pia yaliwashirikisha maofisa ugani wa kata hizo, maofisa wa afya na Idara ya Mifugo na Uvuvi ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambao kwa pamoja waliweka mkakati kuhakikisha chanjo na kinga nyingine muhimu kwa wananchi zinapatikana kwa urahisi hasa maeneo ya vijijini.

Kwa mujibu wa mratibu wa mradi huo, Dk. Ahmed Lugelo, utakuwa wa miaka mitatu kuanzia mwaka huu hadi 2023, ukilenga pia kuhakikisha watu wanaong'atwa na mbwa, wanapata tiba haraka na mwisho kutoa chanjo kwa mbwa wote maeneo hayo ili kukabiliana na kiini cha ugonjwa huo.

Akizungumza wakati wa utoaji chanjo ya mfano ambayo mbwa zaidi ya 200 walichanjwa katika Kijiji cha Kewamamba, Dk. Lugelo alisema maofisa ugani kutoka kata hizo watawezeshwa mafunzo ya mfumo rasmi wa kutumia simu za mkononi kuratibu na kutoa taarifa za kesi za kichaa cha mbwa.

"Kupitia kampeni hii hatua ambazo zinachukuliwa na serikali au halmashauri kupitia kitengo cha mifugo ni kuongeza maradufu hali ya uhamasishaji kuhusu ugonjwa wa kichaa cha mbwa maeneo yote ya ukanda huu.

"Njia ya pekee ya kuepuka ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni kupitia kuchanja mbwa ama kwa njia ya haraka kuchanjwa baada ya kung'atwa ambapo ikiwa mbwa wako atachanjwa, itakugharimu Dola moja tu, lakini ikiwa umeumwa na unahitaji matibabu, itakugharimu Dola 100 kwa chanjo ambazo mtu hupewa kipindi cha wiki mbili hivi," alisema.

Ofisa Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, Dk. Peter Nyanja, alisema jitihada zinahitajika kuhakikisha ugonjwa wa kichaa cha mbwa unaangamizwa kabisa si tu eneo la wilayani, bali maeneo mbalimbali nchini ili kutimiza lengo la kuutokomeza kabisa ifikapo mwaka 2030.

## Mil. 110/- kujenga chumba cha mionzi

**Na Ambrose Mwita,**
TARIME

SERIKALI imetoa Sh. 110m/- kwa ajili kujenga majengo ya mionzi na chumba cha kufulia nguo katika Kituo cha Afya Sirari ili kurahisisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi wanaosafiri umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime, Moses Misiwa, alibainisha kutolewa kwa fungu hilo wakati wa ziara ya kukagua eneo la mradi huo, akiwataka wahusika kuhakikisha fedha zinatumika ilivyokusudiwa.

Misiwa alisema mradi huo ulichelewa kutekelezwa kutokana na kuibuka kwa vikwazo vya mgogoro wa umiliki wa ardhi eneo la utekelezaji wake kati ya kituo hicho na Mahakama ya Mwanzo Sirari, uliomalizwa kwa halmashauri kutenga maeneo mengine.

"Fedha hizi zilipelekwa katika akaunti ya Kijiji cha Buriba kilipo Kituo cha Afya Sirari ambao ndiyo wasimamizi wa mradi huu mwishoni mwa mwaka jana, lakini utekelezaji wake ulikwama kutokana na kuibuka kwa mgogoro wa mipaka ya ardhi kati ya kituo na mahakama na sasa utatekelezwa kwa kuwa kuna maeneo mengine hapa ya ziada," alisema. Diwani wa Sirari, Paul Nyangoko, alisema wakazi wa mji mdogo huo wamekuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu ikiwa pamoja na nchi jirani ya Kenya kutafuta huduma ya mionzi, hivyo mradi huo utawapa nafuu.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Mirumbe Waryoba, alisema taratibu zote za ununuzi ikiwamo kutangaza tenda za kazi kwa uwazi, zinapaswa kuzingatiwa na kudhibiti mianya yote itakayosababisha upotevu wa fedha za umma. "Serikali imekuwa ikisisitiza kwamba lazima fedha za umma zinazopelekwa maeneo hususan ya vijijini, zisimamiwe kikamilifu kwa kufuata sheria na taratibu za serikali ili kuzuia mianya yote itakayosababisha kukosekana thamani ya fedha," alisema.



Baadhi ya wakazi wa Mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakiangalia mafuriko yaliyotokana na bwawa la Kidawash kujaa maji juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Manyara waweka mikataki kuukabili mlipuko Corona

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

MKOA wa Manyara umeanzisha mpango wa dharura kwa wananchi kujikinga na ugonjwa wa virusi vya Corona kwa kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya mkoani humo ili kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema juzi kuwa mkoa huo umejipanga kutoa elimu kwa waataalamu na wananchi ili kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo ulioharibu uchumi wa dunia.

Dk. Kayera alisema wanatumia njia mbalimbali kukabiliana na ugonjwa huo, ikiwamo kutumia vyombo vya habari kutoa elimu kwa wananchi na kutoa elimu kwenye vituo vya afya.

Alisema mkoa huo tayari umeshandaa vifaa na mazingira ya kutolea huduma kwa watu watakaobainika kuwa na maambukizo ya virusi hivyo.

Aliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa serikali imejipanga kutoa huduma hiyo, lakini alisisitiza watu kuchukua tahadhari.

Ofisa Afya Mkoa wa Manyara, Evance Simkoko, alisema kirusi cha Corona kinaenea kwa njia ya kukohoa, kupiga chafya na kwa njia ya maji ambayo siyo rahisi kuonekana kwa macho.

Alisema pamoja na juhudi za serikali za kupambana na ugonja huo, bado kuna tatizo la wananchi kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mlipuko wa ugonjwa huo.

# Waandishi wamkosha waziri hamasa utalii

**Na Allan Isack,** ARUSHA MJINI

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameupongeza uongozi wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC) kwa ushiriki katika uhifadhi wa mazingira, mapambano dhidi ya ujangili na uhamasishaji wa utalii wa ndani.

Kanyasu alitoa pongezi hizo juzi wakati wa ziara ya kikazi kwenye ofisi za APC alipokutana na viongozi wa kamati tendaji ya chama hicho.

Alisema lengo la ziara hiyo ni kuangalia shughuli zinazofanywa na APC na kusikiliza matatizo yanayokikabili chama hicho na kuyatafutia ufumbuzi.

Alisema Mkoa wa Arusha ni kitivo kikuu cha utalii nchini, hivyo amekua akifuatilia taarifa za utalii kwa waandishi wa habari wa Arusha.

Kanyasu alisema waandishi wa habari wa Mkoa wa Arusha wanaongoza kuandika habari za utalii na matokeo yameonekana kuwa makubwa kwenye jamii.

"Arusha mmekuwa na mchango mkubwa sana kwenye suala la maendeleo ya utalii nchini, ukizungumzia ujangili kwa kipindi hiki umeshuka kwa asilimia kubwa, hii imetokana na mchango wenu kuwa mkubwa, mimi kama mwakilishi wa wizara, natumia fursa hii kuwapongeza sana," alisifu.

Naibu Waziri huyo alisema Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kushirikiana na waandishi wa habari nchini kuhamasisha utalii wa ndani na mapambano dhidi ya ujangili unaofanywa na baadhi ya watu wenye nia mbaya na nchi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Claud Gwandu, alimwambia Naibu Waziri huyo kuwa waandishi wa habari wa Arusha wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na uongozi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) katika kutangaza shughuli za utalii.

Alisema chama hicho kipo kwenye maandalizi ya kuandaa maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani yanayofanyika Mei 3 kila mwaka.

Alisema kuwa katika maadhimisho hayo, chama hicho kinatarajia kuzindua televisheni yake ya mtandao na blogu ambazo zitazitumika kuuhabarisha umma masuala ya utalii.

# NHC yachangia mifuko saruji ukarabati shule

**Na Allan Isack, ARUSHA MJINI**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) mkoani Arusha, limekabidhi msaada wa mifuko 100 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni 1.7 kwa Shule ya Sekondari Felix Mrema ili kukarabati miundombinu yake.

Shule hiyo iko Kata ya Daraja Mbili katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Meneja wa shirika hilo mkoani Arusha, Ladislaus Bamanyisa, alisema msaada huo wameutoa kutokana na ahadi yao ya mwaka jana shuleni hapo alipokuwa mgeni rasmi katika mahafali ya kidato ya nne.

Alisema shule hiyo ina uchakavu wa sakafu kwenye baadhi ya madarasa, hivyo mifuko hiyo itasaidia kuboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

Bamanyisa alisema uchakavu huo unatokana na shule hiyo kuwa ya muda mrefu, hivyo uchakavu wa miundombinu yake haukwepeki.

"Mifuko hii ya saruji itasaidia kukarabati sakafu za madarasa yaliyochakaa sana. Pia, tunaahidi kuendelea kutoa msaada zaidi kwa kuwa tukifanya hivi tunamuunga mkono Rais John Magufuli katika mpango wake wa kuboresha sekta ya elimu," alisema.

Bamanyisa alitoa wito kwa taasisi nyingine na mashirika mbalimbali kujitokeza kuchangia elimu hususani katika shule hiyo kwa kuwa kufanya hivyo ni mojawapo ya njia ya kuiunga mkono serikali katika uboreshaji wa huduma ya elimu.

Mkuu wa Shule hiyo, Reginaldo Msendekwa, alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo, akiamini utasaidia kupunguza baadhi ya matatizo yanayoikabili.

Alisema shirika hilo mbali na kukabidhi mifuko ya saruji, pia limetoa Sh. milioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa vioo vya madirisha ya madarasa.

Mjumbe wa Bodi ya Shule hiyo, Hussein Dudu, pia alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo kwa kuwa utasaidia kuboresha miundombinu ya shule hiyo.





Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Peter Serukamba (katikati) na mwenyeji wake Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prof. Said Sife (kushoto), wakiondoka chuoni hapo, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro jana, baada ya kusitisha kikao chao, kutokana na Spika wa Bunge Job Ndugai kusitisha ziara za kamati zote kudumu za Bunge zilizokuwa mikoani na kuzitaka zirudi Dodoma.
**PICHA: GODFREY MUSHI**

# Maaskofu watoa mwongozo kuvikabili virusi vya Corona

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limetoa mwongozo kwa waamini wake nchini kufunga kwa maombi kwa siku mbili, ili Mungu aliepushe taifa na ongezeko la wagonjwa.

Rais wa TEC, Askofu Gervas Nyaisonga, alitoa mwongozo huo juzi wakati wa misa maalum ya kumsimika Askofu mpya wa Jimbo Katoliki Moshi, Ludovick Minde.

Alisema baraza hilo limeafiki kuwapo kwa mfungo huo ili kumwomba Mungu aiepushe Tanzania na janga hilo pamoja na kuwataka waumini kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu mlipuko wa virusi hivyo.

"Katika mwongozo huu, baraza limetangaza siku mbili za maombi kwa ajili ya kumwomba Mwenyezi Mungu atukinge na kutulinda, walioathirika wapone haraka na pia awajalie wataalamu kupata tiba na kinga ya ugonjwa huu," alisema.

Aliongeza kuwa mwongozo huo umelenga kutoa elimu kwa waamini kuzingatia taratibu za kujikinga na ugonjwa huo kama inavyoelekezwa na serikali.

Alisema huduma ya maji ya baraka yanayotumiwa na waamini wakati wa kuingia na kutoka kanisani zitasitishwa kwa muda na kwamba pale kwenye ulazima wa kuyatumia, baraza litatoa mwongozo.

"Hata wakati wa kupokea ekaristi takatifu, waamini watatakiwa kupokea kwa kutumia mikono yao tu na pale ibada inapohusisha mapadri zaidi ya mmoja, watatakiwa kuchovya kwenye divai badala ya kunywa kwa kupokezena," alisema. Alisema mwongozo huo pia unaelekeza kuwa wakati wa misa ya Ijumaa Kuu mwaka huu, waamini hawataruhusiwa kuubusu msalaba na badala yake watatakiwa kuinama kama ishara ya heshima.

Aliwataka mapdri wote na viongozi wengine wa kanisa kuzingatia maagizo hayo na kuhakikisha waamini wanayazingatia ili kujilinda na ugonjwa huo.

Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaac Amani, aliwataka waamini na Watanzania wote kutokufanya mzaha na ugonjwa huo hatari hasa kupitia mitandao ya kijamii.

"Kuna wanaotoa maelezo kupitia mitandao ya kijamii ya kuwa virusi vya Corona haviwezi kumwathiri mtu mweusi, hivyo Waafrika tuko salama, hapo hakuna ukweli wowote, virusi hivi vinawaathiri wanadamu na Waafrika ni binadamu vilevile.

"Ugonjwa huu si ugonjwa wa kuigiza, taarifa mnazoziona na kuzisikia kwenye vyombo vya habari ni za kweli, watu wanakufa na wagonjwa wapo, tena ni wengi, tuache mzaha, tufuate taratibu zinazotolewa za kujikinga," alionya.

Askofu Amani ambaye alikuwa Askofu wa Jimbo Katoliki Moshi kwa miaka 10 kabla ya kuhamishiwa Jimbo Kuu Katoliki Arusha, pia alitoa rai kwa waamini wa Jimbo Katoliki Moshi kumpa ushirikiano Askofu Minde katika utume wake mpya jimboni humo.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ambaye alimwakilisha Rais John Magufuli katika sherehe hiyo, aliipongeza TEC kwa utayari wa kuungana na serikali kukabiliana na virusi vya Corona nchini.

"Tunaamini kama yalivyo majanga mengine na hili pia litapita, ila maadam kwa sasa liko, tuendelee kumwomba Mungu ili atuepushe nalo, nitoe rai kwako Askofu Minde ambaye unachukua uongozi wa jimbo katika kipindi tunapopambana na janga hili, tuungane pamoja katika kukabiliana nalo," alisema.

Katika salamu zake za shukrani, Askofu Minde alimshukuru Mungu kwa kuiwezesha sherehe hiyo kufanyika pamoja na tishio la ugonjwa huo.

"Mimi nilidhani shughuli hii itaahirishwa kutokana na janga hili lililoko, lakini niishukuru pia serikali kwa kukubali iendelee baada ya kuridhika na taratibu pamoja na tahadhari zilizokuwapo," alisema.

Wakati wa misa hiyo, taratibu kadhaa za kiimani za kanisa hilo ilibidi zirukwe ukiwamo utaratibu wa Askofu mpya kupongezwa na Maaskofu wenzake kwa kupeana mikono ambao ulisitishwa na badala yake kusalimiana kwa kuinama kwa heshima.

Pia, utaratibu wa kupeana mikono wakati wa kutakiana amani ulirukwa pamoja na ule wa askofu mpya wa kuwabariki mapdri wa jimbo atakaloliongoza kwa kuwawekea mikono kichwani pia uliachwa na badala yake mapadri hao walifika mbele yake na kuinama kama ishara ya heshima kwake na yeye kuwabariki kwa ishara tu.

## Upatikanaji wa dawa Kibong'oto waridhisha

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

UPATIKANAJI wa dawa muhimu katika Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH) ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na ambukizi, umeimarika kutoka asilimia 70 hadi asilimia 95 mwaka 2019/2020.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, Dk. Riziki Kisonga, alisema juzi kuwa kwa sasa, hospitali hiyo inatoa huduma ya usambazaji wa dawa za tiba ya wagonjwa wa Kifua Kikuu sugu (MDR-TB) walioko katika vituo 341 nchi nzima.

"Tumeanza kuangalia ni jinsi gani tutaweka huduma thabiti na kuisambaza nchini kwa watu waliotibiwa ugonjwa wa kifua kikuu na kupona, lakini bado wanapata matatizo ya kuumwa kifua mara kwa mara ambayo ni sehemu ya magonjwa ambukizi," alisema.

Alisema hospitali hiyo kwa sasa inaendelea kufuatilia mwenendo wa usugu wa vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu katika mikoa minne ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga.

Alisema hospitali hiyo imetangaza kuanza ushirikiano wake na baadhi ya vyuo vikuu vilivyoko katika nchi ya Marekani kama vile Virginia na California San Franscisco katika tiba, mafunzo na utafiti wa kifua kikuu sugu.

Alisema hospitali hiyo pia inashirikiana na nchi za Ulaya katika mafunzo na utafiti. Vyuo hivyo ni Liverpool, St. Andrews (Uingereza), Munich-LMU (Ujerumani), Radboud (Uholanzi), Copenhagen (Denmark), MDR-TB Tarining Centre-Riga (Lativa) na LHL Internation (Norway).

Kuhusu vikwazo vinavyoikabili hospitali hiyo, Dk. Kisonga alisema haina muundo na mfumo wa uendeshaji ambao unaakisi kazi nyingi za utoaji huduma wa kibingwa (rufani).

# Kamati Bunge yakatisha shughuli zake chuo kikuu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

AGIZO la Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuzitaka kamati zote za Bunge za kisekta kusitisha ziara mikoani, limesababisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kukatisha kikao chake muda mfupi baada ya kuingia katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Taarifa ya kutoendelea na kikao hicho ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Peter Serukamba, baada ya kupokea ujumbe maalum wa Spika Ndugai.

Kamati hizo zimerejea jijini Dodoma ikiwa pia zimepita siku tatu tangu serikali ilipozuia mikusanyiko, semina na makongamano ili kukabiliana na maambukizo ya virusi vya Corona.

Kutokana na amri hiyo ya Spika Ndugai, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alilazimika kukabidhi taarifa maalum ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Serukamba.

Baada ya makabidhiano hayo, Serukamba ambaye ni Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), alisema taarifa hiyo itawasilishwa bungeni na itafanyiwa kazi ili kutatua baadhi ya matatizo. Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prof. Alfred Sife, alisema tangu kuanzishwa kwa chuo hicho, ni mara ya kwanza kwa kamati hiyo ya Bunge kufika chuoni hapo. Juzi, Spika Ndugai aliziagiza kamati zote za Bunge za kisekta kusitisha ziara zake na kurejea bungeni Dodoma ambako vikao vyote vitafanyika.

Ndugai alizitaka kamati hizo ambazo zilikuwa kwenye mikoa mbalimbali nchini zikikagua miradi, kusitisha ziara hizo na kurejea jijini Dodoma mara moja.

Tayari Bunge limechukua uamuzi wa kuzuia watu mbalimbali au vikundi ambavyo vimekuwa vikienda kutembelea Bunge kwa ajili ya kujionea shughuli zake kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo.



# Kalemani ataka idadi vijiji umeme wa REA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA MJINI

SERIKALI imeagiza makandarasi wanaotekeleza Mradi wa Kusambazaji Umeme Vijijini (REA), kutoa orodha ya vijiji wanavyopata huduma hiyo kwa wakuu wa wilaya na mikoa ndani ya mwezi huu ili serikali iwe na cha kujibu kwa wananchi.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Alisema utekelezaji wa miradi katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam ambayo ni Kigamboni, Ilala, Mkuranga, Kibaha, Bagamoyo, Chalinze, Kisarawe na Chanika umeanza huku akisisitiza kuwa gharama za kuunganishiwa umeme kwa kila Mtanzania ni Sh. 27,000.

Dk. Kalemani alisema kila mkandarasi anatakiwa kuwasilisha mpango kazi wa kufikisha umeme kwenye maeneo ambayo bado hayajafikiwa kwa viongozi hao ndani ya mwezi huu ili watoe majibu kwa wananchi pindi watakapotaka kujua lini watapatiwa umeme katika maeneo yao.

"Hili litasaidia viongozi hao kuwapatia majibu sahihi wananchi wao wanaowaongoza iwapo yatatokea maswali ya kutaka kufahamu ni lini watafikiwa katika kupatiwa umeme," alisema.

Waziri huyo pia alirejea agizo lake la kuhakikisha nguzo ambazo zimewekwa chini katika maeneo yao ya kazi zisimamishwe sambamba na kufunga transfoma na kukaza nyaya zilizolala ndani ya mwezi huu.

"Mkandarasi na msimamizi wa mradi atakayeshindwa kufuata maelekezo haya, atachukuliwa hatua stahiki kwa kuwa wananchi wanataka umeme ili kuongeza chachu ya maendeleo," alisema.

Alibainisha kuwa hadi sasa, vijiji 91,000 vimepatiwa umeme ndani ya miaka nne ya serikali ya awamu ya tano na kuchochea mafanikio makubwa katika kuelekea uchumi wa viwanda.

Alisema katika mpango unaoendelea, wamebakiza vijiji 1,822, ambavyo vinatarajiwa kupelekewa umeme kuanzia Juni mwaka huu ili ifikapo Juni mwakani, viwe vimepatiwa huduma hiyo muhimu.

# Jafo aagiza wanafunzi wote waliokosa usafiri kusafirishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA MJINI

WAZIRI wa Nchi,Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wakuu wa shule kuhakikisha wanasafirisha wanafunzi waliokosa usafiri badala ya kuwaacha wazagae ovyo kwenye vituo vya mabasi.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari kwa siku 30 kuanzia siku hiyo kutokana na tishio la ugonjwa wa Corona. Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Waziri Jafo alisema baadhi ya mikoa wanafunzi wameonekana kuzagaa na wengine kulala kwenye vituo vya mabasi kutokana na viongozi hao kutotekeleza agizo la kuhakikisha wanasafiri kwa usalama na amani hadi makwao.

Jafo alisema Katibu Mkuu Tamisemi alishaandika barua kupitia ofisi za mikoa kuhakikisha unawekwa utaratibu mzuri kuanzia Machi 17 hadi 20 mwaka huu wanafunzi kurejea nyumbani.

Waziri Jafo alisema kuna baadhi ya maeneo utaratibu huo haukufanyika kwa kuwa hadi jana wanafunzi wameruhusiwa kwenda kwenye vituo hivyo kutafuta magari wenyewe, jambo ambalo ni kinyume cha maelekezo yaliyotolewa.

"Kama kuna shida, wakuu wa shule wawasiliane na wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama ambao ni wakuu wa wilaya, haileti picha nzuri kuona wanafunzi wamezagaa vituoni wakitafuta usafiri, jambo ambalo linadhihirisha kuwa wakuu wa shule hawakujipanga vizuri," alisema.

Alitoa pongezi kwa Mkuu wa Shule ya Kilakala iliyoko Morogoro na Mkuu wa Shule ya Sekondari Dodoma kwa kuweka utaratibu mzuri wa kusafirisha wanafunzi hao.

"Kilakala alihakikisha wanafunzi wake wote anawakodia mabasi yanawachukua shuleni na hadi leo (jana) alikuwa amebaki na wanafunzi 30 tu ambao anawasafirisha, pia Dodoma yeye hata wanafunzi wasiokuwa na nauli alikodi magari kuwasafirisha bila nauli na kuwataka wazazi watume kwake nauli hizo ili alipe gharama za usafiri," alisema.



Wakazi wa Mtaa wa Surugai, Kata ya Ipagala, jijini Dodoma, wakitoa nje vyombo baada ya nyumba yao kujaa maji kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mtambo wa kusaga mawe kwenye figo waanza kazi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MTAMBO wa kuvunja mawe kwenye mfumo wa mkojo, hususan kwenye figo (Extracoporeal Shock Wave Lithotipsy), ambao ni wa kwanza nchini, umeanza kutoa huduma katika Hospitali ya Benjamin Mkapa mkoani Dodoma.

Uvunjaji huo unafanywa kwa kutumia mionzi badala ya upasuaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema juzi kuwa mtambo huo uko tayari kuanza huduma hiyo na kwa nchi nzima upo kwenye hospitali hiyo pekee.

"Tunashukuru serikali kwa kuleta vifaa tiba vya kisasa na vya gharama kubwa kwa ajili ya wananchi wake, tumekuwa tukitoa huduma ya uvunjaji mawe kwa upasuaji, lakini huu mtambo unatumia mionzi ambayo si mikali sana.

"Mgonjwa anawekwa kwenye mashine na inaelekezwa kwenye jiwe, yenyewe ndiyo inapasua kwa kutumia mionzi na vipande hivyo vinatoka kwa njia ya mkojo," alisema.

Aliishukuru serikali kwa kufunga mtambo huo wenye gharama ya Sh. bilioni 2.5 na kwamba wamebaini Kanda ya Kati inaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wenye mawe kwenye mfumo wa mkojo.

"Takwimu za hospitalini hapa kwa wagonjwa wa mfumo wa mkojo zinaonyesha wagonjwa wanaoongoza ni tezi dume inashika namba moja na inayofuatia ni mawe kwenye kibofu cha mkojo," alisema.

Alisema hospitali hiyo inahudumia wagonjwa wanne hadi watano kwa wiki wenye mawe na kwa mwaka wagonjwa zaidi ya 50 wanafanyiwa upasuaji wa kuondoa mawe.

"Uwapo wa mashine hii ambayo imenunuliwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni 2.5, utasaidia wananchi wa Kanda ya Kati na Watanzania wenye shida ya mawe kwenye kibofu cha mkojo, mawe yanasababisha figo kutofanya kazi na mashine imewekwa ili kuokoa figo zisiharibike," alisema.


Alisema kuna haja kufanya utafiti zaidi kujua sababu za kanda hiyo kuongoza kwa kuwa na wagonjwa wenye mawe, lakini baadhi ya wataalam wanasema inasababishwa na hali ya hewa ya ukanda huo na watu kutokupenda kunywa maji.

Daktari Bingwa wa Mfumo wa Mkojo, Dk. Okoa Sukunala, alisema nchi zingine kwa wagonjwa wenye tatizo hilo, upasuaji unafanyika chini ya asilimia moja lakini wanatumia mashine ya aina hiyo kusaga mawe.

"Njia tuliyokuwa tunatumia ilikuwa inamlazimu mgonjwa kulazwa wiki nzima wodini," alisema.

Alisema zipo sababu mbalimbali ikiwamo ya kimazingira hasa mazingira ya joto na jangwa, tabia za watu kutokunywa maji ya kutosha na kurithi, zinazosababisha mawe kutengenezeka kwenye mfumo huo.

"Sababu nyingine ni umri miaka 20-40, ndiyo umri wa kutengeneza maji na wanaume ndiyo wapo kwenye hatari zaidi kupata mawe kuliko wanawake," alisema.







Ofisa Ufuatiliaji Tathmini wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Muhammed Khatiba, akizungumza na wanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mufti atoa angalizo sala mlipuko Corona

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

OFISI ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, imewataka maimamu na viongozi wa misikiti kuhakikisha wanafupisha visomo vya sala na hotuba za Ijumaa, ikiwa ni sehemu ya tahadhari ya kujikinga na mlipuko wa virusi vya Corona.

Katibu wa Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya tamko la Ofisi ya Mufti Mkuu kuhusu utaratibu wa ibada na tahadhari kwa ugonjwa huo.

Alisema maimamu wanatakiwa kufupisha visomo vya ibada ya sala, akipendekeza kusoma visomo vifupi, hatua ambayo itawafanya kuchukuwa muda mfupi kumaliza ibada.

Alisema katika sala ya Ijumaa, maimamu wanatakiwa kufupisha ibada hiyo hadi dakika 20.

"Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar inaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kupambana na janga la ugonjwa wa Corona.

"Waislamu tunatakiwa tukubaliane na mabadiliko hayo ikiwamo kufupisha ibada pamoja na kuomba dua za kuondoka kwa janga hilo," alisema.

Tamko hilo la Ofisi ya Mufti limesisitiza kuendelea kufanyika kwa sala ya Jamaa ambayo kwa kawaida hukusanyisha idadi kubwa ya waumini kwa wakati mmoja.

Mfaume aliwataka maimamu kuhakikisha kwamba baada ya kumaliza sala, wanapata wasaa wa kuleta Istighfari (maombi maalum) pamoja na dua ya Kunuti ili kumwomba Mungu kuondokana na janga hilo.

"Waislamu tunao utaratibu wa kuomba dua ya pamoja wakati yanapotokezea majanga makubwa kama ugonjwa huu Corona. Tunawaomba maimamu watumie nafasi hiyo kuliombea taifa liepukane na janga hili," aliagiza.

# Kamati yabaini tatizo mtihani wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

KAMATI ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, imelitaka Baraza la Mitihani la Taifa kuhakikisha linawapa elimu walimu wanaosimamia mitihani na kuwatambuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili nao wafanye katika mitihani hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanaasha Khamis Juma, alitoa rai hiyo alipokutana na uongozi wa baraza hilo kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa majukumu yao.Alisema yapo baadhi ya malalamiko kwa wasimamizi wa mitihani kushindwa kutambua uwapo wa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mitihani na kuchukulia wanafunzi wote ni sawa.

Aliwataka wasimamizi wa mitihani hiyo kutoa nafasi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kuhakikisha wanafanya na kumaliza mitihani yao na badala ya kuwekwa kundi moja na wanafunzi wengine.

"Tumepokea malalamiko kwa baadhi ya wazazi na wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata matatizo, hakuna anayewajali wakati wa kufanya mitihani yao ya taifa, wanachukuliwa sawa na wanafunzi wengine.

"Wa wanafunzi hawaoni, huwezi kumlinganisha na anayeona, kwa hivyo wanatakiwa kuzingatia mahitaji yao," kiongozi huyo wa kamati aliagiza.

Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani Zanzibar, Zubeir Juma, alisema kuanzishwa kwa baraza hilo kwa kiasi kikubwa kumerahisisha kutoa matokeo ya mitihani kwa wanafunzi wa darala la sita na kidato cha pili pamoja na kufanya uchambuzi wa matokeo ya mitihani.

Alisema baraza limefanikiwa kujenga uhusiano mzuri na halmashauri za wilaya na mabaraza ya miji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ugatuzi wa kufikisha huduma muhimu za elimu.

"Baraza la Mitihani la Zanzibar limejenga uhusiano mzuri kwa shule za elimu ya sekondari hadi msingi ambazo kwa sasa zipo katika mpango wa ugatuzi wa kufikisha huduma hizo katika mabaraza ya miji na halmashauri za wilaya," alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, aliwataka walimu kuwatambua wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao sera ya elimu inawatambua na kuwajali.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tumeanzisha elimu mjumuisho ambayo huwatambua wanafunzi wote wenye mahitaji maalum kufaidika na fursa za elimu zinazotolewa na wizara," alisema.

# Mradi ujenzi kijiji utalii washika kasi

**Na Mwandishi Wetu,** UNGUJA

SERIKALI ya Zanzibar imesema imeridhishwa na hatua iliyofikiwa katika mradi wa kijiji kikubwa cha kitalii kinachojengwa na Kampuni ya Pennyroyal Matemwe Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Timu ya Mamlaka ya Uwezeshaji Miradi ya Uwekezaji Zanzibar (Zipa) na taasisi kadhaa za serikali, iliutembelea mradi huo kukagua maendeleo ya awamu ya kwanza ya ujenzi wake na kusema serikali inafurahishwa na kasi yake.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo na kupata maelezo kutoka kwa uongozi wa Zanzibar Amber Resort, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Shariff Ali Shariff, alisema azma ya serikali inayoongozwa na Rais Ali Mohamed Shein, ni kuona Zanzibar inakuwa na utalii wa daraja la juu utakaosaidia kukuza uchumi.

Alisema hatua iliyofikiwa ambapo nyumba kadhaa zitakazokuwa na vyumba vinavyojitegemea inaendela vizuri, hivyo kuondoa wasiwasi wa watu wenye pingamizi kuwa mradi huo mkubwa hautafanikiwa.

Shariff aliyekuwa amefuatana na watendaji wa mamlaka za ardhi na mazingira, alisema ni ukweli usiopingika kwamba kuongezeka kwa uwekezaji mkubwa kama huo katika visiwa vya Zanzibar, kutafungua fursa za ajira kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya miradi.

"Kutokana na ukubwa wake, miradi kama hii inaweza kuchukua muda mrefu kukamilika, lakini manufaa yake yatajumuisha wananchi wengi pamoja na serikali kutunisha mfuko wake wa kodi ambazo ni muhimu kwa maendeleo," alisema.

Aliahidi kuvifanyia kazi vikwazo vya kiujenzi vinavyoukabili mradi huo, huku akiutaka uongozi wa kampuni hiyo kuiandikia mamlaka anayoiongoza juu ya mahitaji yenye umuhimu ambayo upatikanaji wake unakwama.

Aliutaka uongozi wa Zanzibar Amber Resort kuisimamia vyema zaidi kampuni inayojenga kijiji hicho ili kuhakikisha awamu ya kwanza inafikia hatua nzuri na kuwahi kuwekwa jiwe la msingi na Rais Shein kabla hajamaliza kipindi chake madarakani.

"Kama tunavyojua, Mheshimiwa Rais ameuafiki kwa matumaini makubwa mradi huu, na ndiye aliyesimamia upatikanaji wa fursa hii, hivyo tufanye hima ili naye awe sehemu ya mafanikio kwa mkono wake," alisisitiza.

Meneja wa mradi huo, Murtaza Hassanali, alisema kwa upande wa malighafi za ndani, rasilimali ya mchanga ndiyo kikwazo kikubwa kikachowapunguza kasi katika ujenzi huo. Alisema katika awamu ya kwanza, wameomba tani 15,000 za mchanga kutoka Idara ya Maliasili Zisizorejesheka, lakini waliambulia tani 100, huku wakitakiwa kuandika maombi mengine kila wanapohitaji mchanga wa ziada.



**MWANA FA**

Soma UK.14

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI MACHI 21, 2020



# JuX, Huddah wamelianzisha tena

Soma UK.14

BASI SAWA



## Pole Mwana FA, Mungu atakupigania

RAPA anayependwa kutokana na aina yake ya mashahiri, Mwana FA, ametangaza kupata virusi vya corona.

Akitumia video fupi, Mwana FA, amesema tatizo hilo amelipata akiwa nchini Afrika Kusini, aliporejea aliamua kupima na kukutwa ameathirika na ugonjwa huo.

Niliporejea kutoka Afrika Kusini, nilihisi joto linapanda na kushuka na ndipo nilipoamua kwenda kupima na kuonekana nimemabukizwa," amesema Mwana FA

Amewaonya Watanzania kwamba ugonjwa huo upona unampata kila mtu, hivyo ni muhimu kufuata kanuni za afya.

Hata hivyo, Waziri wa Afya, Watoto na Ustawi wa Jamii, Ummy Mwalimu, amempongeza msanii huyo kwa hatua yake hiyo na kumwambia yeye ni kijana jasiri.



## Dully Sykes hujui kupenda sawa na upofu?

MKONGWE wa BongoFleva, Dully Sykes, amesema tukio la kuachwa lilimfanya kuchanganyikiwa na kushindwa kufanya kazi na majukumu yake.

Amesema tukio hilo lilimkuta pale mama mtoto wake alipoamua kuondoka na kisha aliamua kugawa kila kitu na kusababisha hadi leo alale chini.

"Mama wa mtoto wangu wa tatu aliniacha, kwa sababu tulikuwa tunaishi wote kwa muda mrefu bila ya kufunga ndoa, alivyoondoka sikuamini na kuniacha nimeathirika hadi nilichanganyikiwa.Meza ya vipodozi aliyokuwa anatumia nikaigawa, kitanda ambacho tulikuwa tunakilalia nikakigawa pia hadi leo nalala chini" ameeleza Dully Sykes.



# JUX, HUDDAH WAMELIANZISHA TENA

MASHABIKI na wapenzi wa mwanamuziki wa RnB, Juma Jux, wameanza kumchimbachimba msanii huyo wakitaka kujua kama mrembo wa Kenya, Huddah The Bosschick, ni mpenzi wake.

Kumekuwepo na fununu kwamba wawili hao wana uhusiano wa kimapenzi tangu siku nyingi.

Hivi karibuni kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram ambapo Jux amepost picha, kisha Huddah akaja kujibu kwa kuandika "Yaani sasa hivi Zanzibar ni sehemu bora ya kukaa rafiki yangu, nitakuona huko".

Baada ujumbe huo, Jux naye akamjibu kwa kuandika "Kabisa rafiki yangu ahsante kwa kuniongezea mwanga rafiki yangu".

Ikumbukwe tu taarifa za wawili hao kuwa na uhusiano zilinza kuripotiwa tangu walipoonekana wapo katika hoteli moja huko visiwani Zanzibar, ambapo kila mtu alikwenda kupumzika kivyake.

## INSTA-TWITTER





**Nachukua** nafasi kukuwish kwenye albamu yako mpya.Nakumbuka ilikuwa ni ndoto yako na hatimaye umekamilisha. Tumetoka mbali, tumepitia mengi, tumegombanishwa sana. Na hii yote ni kwa sababu ya kiburi changu. Ukweli haufichiki siwezi kuacha kufurahia unachokifanya na unavyopambana. **Jackline Wolper.**



**Kuna** mijinga itaona unajipendekeza au watakutukana, ila kiukweli nimependa hili. Hata kama mmeachana hamtakiwi kuwa maadui na mkizingatia wote ni vijana. Wote tupo kwenye sanaa, cha muhimu ni kuombeana mema. Safi sana Jack wangu, umefanya jambo zuri kuliko kuweka mizigo moyoni Jackline Wolper nakupenda sana-**Shamsa Ford.**



## Muna Love wakati mwingine shetani hajaribiwi

MUNA Love amewashangaza watu wengi baada ya kudai tukio lake la kutangaza kujitoa mitandaoni na kubadilisha dini lilitokana na kupitiwa na shetani.

Muna Love amesema wakati anatangaza kujitoa mitandaoni kisha kurejea baada ya siku mbili, alikuwa anajaribiwa na shetani ambaye alikuwa anamdanganya na kumyumbisha lakini amemshindwa.

"Suala la kujitoa mitandoni niliona shetani alikuwa anataka kuniyumbisha na kunidanganya, nikaona hapana acha nimuaibishe nirudi, naweza kuishi bila mitandao lakini mwisho wa siku ina faida na mimi kwenye kutangaza biashara zangu" ameeleza Muna Love.




# MUUMINI ARUDI KIVINGINE

KATIKA kutafuta maisha hakuna kukata tamaa, ndivyo anavyofanya mwanamuziki mkongwe wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, baada ya kuibuka upya akiwa na bendi ya Shadai 'Wana Tikisatikisa'.

Muumini ni miongoni mwa wanamuziki waliopopotea na kurejea tena katika muziki huo.

Mwaka 2001, nyota yake iling'aa akiwa katika Double M Sound ambayo ilivuma kwa kipindi kifupi kisha ikayumba na hatimaye kupotea.

Katika muungano wake na Ally Choki, walianzisha bendi ya Double Extra ambayo nayo haikudumu na kulazimika kwa nyakati kuhama bendi moja hadi nyingine bila ya mafanikio.

Sasa ameibuka upya kupitia bendi ya Shadai ambayo itazinduliwa rasmi Machi 28 jijini Dodoma.

"Sijakata tamaa, kwani katika kutafuta ni muhimu kukomaa hadi kieleweke, hivyo nitaendelea kupigania muziki wa dansi hadi mwisho," amesema.





>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Haya** nichambeni nimewaruhusu-**Amber Lulu.**



**Amani** humpa mtu tabasamu usoni Ingawa yawezekana ukweli wa maisha yako umeficha maumivu mazito, ila kitu pekee kinachoweza kukupa matumaini ya kuendelea ni Imani ya kweli na kujikabidhisha kwa Mungu. kwa sababu kimbilio la kila mnyonge ni Mungu pekee-**Amber Rutty**.



**Kinga** ni bora kuliko tiba ndugu zangu na hii sio fashion tafadhali tuchukue tahadhari kwa ugonjwa wa Corona, Mungu atatulinda inshallah-**Shilole**.

# Kuumbe!



# KORONA KILA KONA

## HASARA WASANII KIBAO WAVUNJA MATAMASHA WAPO WALIOUZA TIKETI

BAADHI ya wasanii nyota duniani wametangaza kusitisha shughuli zao baada ya mnlipuko wa ugonjwa wa corona kutishia karibu kila taifa.

Wasanii hao wamechukua hatua hiyo baada ya nchi nyingi ikiwamo Tanzania kupiga marufuku mikusanyiko ya watu ikiwa ni harakati ya kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo.

Mwanamuziki, Nasib Abdul maarufu Diamond Platnum kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram ametangaza kuahirisha matamasha yake ya Ulaya.

Awali Diamond alikuwa na mpango wa kufanya maonyesho nchini Uswiss.

Mwanamuziki wa Nigeria Davido Adeleke pia amelazimika kuvunja tamasha lake alilotarajiwa kulifanya nchini Marekani.

Licha ya tiketi za tamasha hilo kuuzwa, imemlazimu kuwaomba radhi mashabilki na wapenzi wa muziki wake kwamba hataweza kuburudisha tena.

"Ninasikitishwa na kuvunja tamasha, licha ya kushuhudia kuuzwa kwa tiketi zote za safari bora ya kimuziki hadi sasa, lakini kuahirisha ni kitu sahihi kukifanya hivi sasa kwa afya na usalama wa mashabiki wangu" umeandika Davido kupitia mtandao wake wa Instagram

Nchini Kenya moja ya burudani iliyotangazwa kuahirishwa ni vichekesho vya Churchill

Daniel Ndambuki, al maarufu Mwalimu King'ang'i amefuta maonyesho yake kufuatia mlipuko huo katika jiji la Nairobi.

Mchekeshaji maarufu wa Televisheni nchini Marekani Trevor Noah ameahirisha kuishirikisha hadhira katika kipindi chake kutokana na hofu ya corona.

Mchekeshaji huyo kutoka kutoka Afrika Kusini, hualika mashabiki wake katika kipindi chake cha kila siku ya Alhamisi kinachopeperushwa moja kwa moja, akisema hawezi kufanya hivyo kutokana na kuwepo kwa ugonjwa huo.

Trevor Noah amesema kipindi chake cha Daily Show kililazimika kutekeleza jukumu lake la kukabiliana na virusi vya corona.

Matamasha mengine makubwa yamefuata mkondo huo nchini Marekani.



# Wasanii wanavyolia na janga la Corona

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA kwa sasa iko kwenye sintofahamu kutokana na mlipuko wa kirusi kilichopewa jina la COVID-19 kinachosababisha mafua makali na homa ya corona.

Tayari vimesambaa zaidi ya nchi 100 duniani, huku watu 179,111 wakiwa wamshaambukizwa na kati yao 11,525 wakiwa wameshafariki dunia.

Nchini , hadi safu hii inakwenda mitamboni, kulikuwa na taarifa iliyothibitishwa na serikali kuwepo kwa wagonjwa watatu ambao wote wametokea nje ya nchi hii.

Ni kama vile dunia imesamama kwani shughuli mbalimbali hasa zenye mikusanyiko zimesimamishwa. Shughuli hizo ni kama vile burudani, michezo, mikutano na hata mikusanyiko ya watu.

Nchini Tanzania, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, pamoja na mambo mengine, alisimamisha shughuli zote za burudani na michezo, pamoja na shule zote nchini kwa muda wa simu 30, ili kukabiliana na maambukizo mapya ya ugonjwa huyo.

Kwa kuunga mkono jambo hilo, wasanii mbalimbali nchini wameshaanza kuingia studio kutoa nyimbo zinazohusu ugonjwa huo.

Lengo ni kuelimisha wananchi kujikinga na kuwa na tahadhari, pamoja hatua za kuchukua pindi wanapoona dalili na kukabiliana nazo.

**Rayvanny-Corona**

Msanii maarufu nchini Rayvanny, tayari ameshatoa ngoma yake inayozungumzia juu ya ugonjwa huo.

Katika wimbo huo anasema kuwa habari zimesambaa kote duniani kuhusiana na ugonjwa huo.

Mpaka sasa hauna tiba ya uhakika na unaweza kuua pia. Msanii huyo anasema kuwa ni wakati wa Wabongo kumuomba Mungu kwani hapa kwetu wengi ni masikini, lakini anwataka watu kuchukua tahadhari wa kunawa mikono na kuepuka mikusanyiko.

**Mzee wa Bwax-Corona**

Huyu ni msanii wa muziki wenye mahadhi ya singeli. Naye ameingia studio na kuja na ngoma ya 'Corona'.

Anasema kuwa ugonjwa huu ni balaa. Moja kati ya beti za wimbo huu ni kwamba anamkataza rafiki yake asimpe mkono anaogopa Corona. Mpenzi wake asimpige busu anaogopa Corona.

Hii yote ni sanaa katika kuelezea zile njia ambazo zinaweza kusababisha kuambukizwa ugonjwa huo.

**Susumila ft Mbosso-Corona**

Wasanii hawa wawili wameungana na kuingia studio, wanatoa ngoma moja ya Corona.

Wamejikita zaidi katika dalili za ugonjwa wenyewe kuwa mgonjwa anakohoa huku anatetemeka.

Nao wamekuwa moja ya wasanii wachache ambao wameamua kuelimisha wananchi ambao ni mashabiki wao kuhusu ugonjwa wa Corona.

**Bethael Nsumyi-Corona**

Huyu ni mwimbaji wa nyimbo za Injili. Naye hakuwa nyuma, kwani ametoa wimbo unaohusiana na Corona.

Naye anajikita kwenye kuelimisha wananchi wasisalimiane kwa mikono au kukumbatiana.

Lakini pia anasikitika kuwa Watanzania ni watu wa amani na utulivu ndiyo jadi yao na wamezoea kusalimiana na mikono na kukumbatiana. Anajiuliza sasa Wabongo wataishije na utamaduni mpya ya kusalimiana bila kugusana? Hata hivyo anawataka Watanzania wajihadhari.

**Amani na Upendo Group-Corona**

Hili ni kundi lenye maskani yake Tabata jijini Dar es Salaam. Linapiga muziki wake kwa staili ya kwaya.

Kundi hilo nalo halikuwa nyuma kwani wametoa wimbo unaohusiana na ugonjwa huo, likiwataka watu kujihadhari, huku pia moja kati ya Wabongo wanapaswa wajiepushe ni kuwa mbali na mgonjwa mwenyewe, au kuwa makini mtu ambaye ana historia ya kusafiri nje ya nchi, na hasa kwenye nchi zenye historia ya ugonjwa huo, ingawa kwa sasa ni zaidi ya nchi 100 dunaini zina wagonjwa.



# IMETOKEA

## Farah binti mwenye ugonjwa wa kuhuzunisha

FARAH Khalek (33) raia wa Kenya, anakabiliana na ugonjwa wa ngozi ambao umebadilisha muonekano wake wa sura na kufanya wengi wasimtambue.

Ugonjwa huo unaojulikana kama Scleroderma umempata na kusababisha ngozi yake kuwa ngumu na kukakamaa sana na endapo mtu akiupata ngozi yake inabadilika kiasi ambacho huwezi kumtambua kwa haraka.

Farah alizaliwa akiwa na sura nzuri na iliyomvutia kila mtu.

Akiwa ni msichana wa pekee katika familia ya watoto watatu kwa wazazi wake, anasema alipata malezi mazuri na alipendwa zaidi.

"Wazazi wangu na ndugu zangu walinidekeza tangu nikiwa mtoto mdogo, kwa hiyo mimi nilikuwa katika mazingira ambayo nilihisi upendo na kukubalika" alisema Farah.

Farah anaeleza kuwa akiwa na miaka 17 hali yake ilianza kubadilika wakati akiwa sekondari.

Anasema kuwa ugonjwa huo ulianza kwa kuonyesha dalili mikononi kwa ngozi yake kuwa ngumu huku kucha zake zikibadilika rangi na kuwa bluu inayokaribia weusi

"Nilikuwa na hasira nao sana, wakati huo nakumbuka niligombana na mama yangu nikawa napigana kila wakati huku nalia tu kutokana na sura yangu ilikuwa inanitisha hata mimi mwenyewe niliogopa " Farah alisimulia.

Farah anasema kuwa kila siku mwili wake ulichukua muonekano usiokuwa wa kawaida na binadamu wengine, ukijikunja.

Walipokwenda hospitalini, anasema wazazi wake walishauriwa watafute matibabu nje ya nchi, na hapo ndipo waliamua kwenda nchini India.

Walipofika huko baada ya kufanyiwa uchunguzi waligundua kuwa ana ugonjwa ambao hauna kinga, unaojulikana kama 'scleroderma'.

Farah ameiambia BBC kuwa tangu akiwa na miaka 17 mpaka sasa mwili wake umepitia mabadiliko mengi.

Muonekano wake wa zamani na wa sasa huwezi kujua kwamba ni mtu mmoja, kwani Scleroderma imembadilisha sana sura.

Athari nyingine za mwili ni kutokana na ugumu wa viungo vya mwili ikiwamo mikono yake kukosa nguvu kiasi hawezi kuchana hata nywele zake kwa kutumia kichanuo wala kushika kifaa chochote .

Shughuli ambazo binadamu huzichukulia kuwa za kawaida kama kusimama , kuinama , kuandika kwa kalamu, sio jambo rahisi kwake Farah .

"Mambo ya kawaida kama kuchana nywele zangu siyawezi, kwa kuwa viungo vyangu vya mkono vimekuwa vigumu na kushikana, kwa hiyo inabidi mama anisaidie kila siku," anasema.

Pia Farah anaeleza anapata changamoto kuishi na hali hiyo kwenye jamii inamnyanyapaa pale anapotoka nje ya nyumba yao.

Anasema watoto walikuwa wanamuogopa kwa sababu ya sura yake licha ya yeye mwenyewe kujaribu kuwapa tabasamu lakini bado waliogopa.

"Kwa kweli siku hizi mimi hucheka tu watu wanaponikodolea macho njiani, kwani sina la kufanya " anasema farah.

Farah anakiri kuwa ilichukua muda kwake kukubali kujiangalia kwenye kioo.

Sura yake imepelekea watu kumuita majina ya ajabu, wakati mmoja anasema kwenye mitandao ya kijamii walimpa majina anbayo si mazuri.






## JOKA LA KIJIJI
## Dhambi ya mmoja pekee inavyotesa familia nzima

**Na Adam Fungamwango**

KOSA au dhambi ya mtu mmoja tu, inaweza kutesa au kuteketeza familia nzima. Hilo lipo dhahiri. Inawezekana tatizo linalompata yoyote yule leo, lilisababishwa na baba, mama, bibi, au babu miaka mingi nyuma.

Wakati mwingine Mungu huadhibu familia, kutokana na matendo mabaya yaliyofanywa na mmoja kati yao, hata kizazi cha nne au cha tano nyuma.

Kuna baadhi ya familia zimekuwa na magonjwa ya kurithi, ugumba au mkosi wowote ule kwa baadhi ya watu au mwanafamilia kwenye familia hiyo, lakini chanzo ni mmoja kati ya watu wa kizazi hicho, kutoka upande wa baba au mama.

Sultan Tamba, mmoja wa waandishi wakubwa wa riwaya, pamoja na uandishi wa filamu, ameliona hili na kuja na kitu kiitwacho 'Joka la Kijiji'.

Filamu hii inafundisha kuwa wakati mwingine madhila yanayotupata binadamu, inawezekana yamesababishwa makosa ya vizazi vyetu miaka mingi nyuma.

Tausi na wifi yake Zaria wanakwenda kisimani kuteka maji. Huko wanakutana na chatu mkubwa. Anammeza Zaria na kutoweka. Tausi anakimbia hadi dukani kwa mama yake na kumweleza jambo hilo. Mama yake badala ya kushtuka na kulichukulia jambo hilo kama ni janga la kijiji, anamkanya binti yake asimwambie mtu yoyote kuhusu jambo hilo. Tausi anashangaa, lakini anatii amri.

Madebe anamtafuta mchumba wake Zaria, lakini hamuoni. Wazazi wa Zaria wanamsaka binti yao, lakini haonekani. Wapo wanaodhani kuwa ameliwa na wanyama wakali, lakini wengine wakadhani huenda ametoroka kijijini na kwenda mjini kwa bwana.

Madebe kwa mara ya kwanza anashuhudia rafiki yake akimezwa na chatu huyo mkubwa. Anakwenda kumwambia mama yake. Lakini mama yake anamkanya juu ya kuongea hovyo juu ya joka lile. Hii inampa wasiwasi Madebe kuwa kuna kitu nyuma ya pazia juu ya haya yanayotokea.

Siku isiyo na jina anamshuhudia mwenyewe laivu akitoka ndani ya nyumba yao na kuelekea porini, lakini baadaye akarejea na kuingia ndani humo humo.

Ilibidi Madebe amkabili baba yake wa kambo, na kumuuliza jambo hilo. Mzee naye alikuwa hana habari yoyote ile.

Madebe akambana dada yake Tausi juu ya kile kinachotokea na ndipo binti huyo alipomwambia laivu kuwa joka au chatu yule anafungwa na mama yao mzazi na anaishi ndani mle mle.

Hii inamuogopesha mno Madebe na hata baba yake wa kambo. Wanaamua kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kumuelezea.

Mwenyekiti huyo, ndiye baba wa Zaria aliyemezea na joka. Anambana mama huyo aeleze ukweli ili wasaidiane kuondoa tatizo, la sivyo ataita wanakijiji wote na kueleza ukweli wote kuwa anafuga joka ambalo tayari limemeza baadhi ya watu kijijini hapo.

Mama Tausi anaanza kueleza ukweli kuwa joka lile analifuga yeye, lakini si kwa kupenda.

Miaka mingi iliyopita alimuua mume wake ambaye ni baba wa kina Madebe na Tausi ili tu arithi mali nyingi alizokuwa nazo.

Staili aliyomuua ni kumtumbukiza kisimani, siku alipomuomba aende akamsaidia kuchota maji.

Lakini kwa bahati mbaya alikosea baadhi ya masharti na marehemu huyo kugeuka mzimu ambao ni joka hilo ambalo limekuja kuishi ndani, huku likiwa haliwamezi Madebe na Tausi kwa sababu ni watoto wake.

Hata hivyo mama huyo alisema kuwa dawa ambayo ikifukizwa anatoka kwenda kutafuta chakula.

Makubaliano ya wote ni kwamba dawa hiyo atumike ifukizwe hadi kutoka hapo nyumbani hadi kwenye kisima ili arudi humo.

Na kweli ilisaidia kwani, joka lilitoka ndani na kufuata harufu hiyo hadI kisimani likaingia. Dawa iliyobaki ikamwagiwa ili liendelee kubaki humo.



# UNAWEZA KUKUBALI PARIS JACKSON ATILIA SHAKA KUKAA KARANTINI

SAKATA la kusambaa kwa virusi vya corona limeathiri sekta nyingi duniani na moja ya sekta iliyoathirika ni sanaa, ambapo wasanii mbalimbali wameamua kukatisha matamasha yao kwa kuhofia kuambukizwa ugonjwa huo na wengine kutangaza rasmi kwamba wameambukizwa.

Kwa wale waliopima na kufahamu tayari wana virusi hivyo, wameamua kujitenga na jamii ikiwa kujifungia ndani ili kuepesha uwezekano wa kuwaambukiza wengine.

Hata hivyo, mtoto wa aliyekuwa Mfalme wa Pop duniani, Michael Jackson, Paris Jackson, amesema hatua ya kujitenga katika kukabiliana na ugonjwa huo unazidisha tatizo.

Paris Jackson ambaye ni mtoto wa kwanza wa MJ, anasema watu wanaweza kukabiliwa na upweke wakati wanapotengwa na kuwekwa kwenye karantini wakati wakipatiwa matibabu.

Akizungumzia suala hilo, anasema ni jambo gumu kwa mtu aliyezoea kuona magari na harakati nyingi za kibinadamu kuzuiwa ghafla.

Amesema kama kuna uwezekano watalamu wangeweza kutoa tahadhari na njia zinazofaa, kuliko mtu mwenyewe kujiweka katika karantini ndani na kumsababishia upweke.

Paris inasema wanadamu kwa asili, ni viumbe vya kijamii, ni jambo gumu kuwa katika hali ya sasa ya kuwa kuzuizini na akili yake kupingana na hisia zake za uhuru.

"Ni jambo gumu kukaa peke yako kizuizini, nafikiri ingetafutwa njia nyingine ambayo haiwezi kuleta athari zingine kama upweke pale mtu anapokuwa ndani," anasema Paris.

Baadhi ya mastaa wamethibitisha kupata ugonjwa huo na kujiweka hadharani katika mitandao ya kijamii.

Virusi hivyo vya corona ambavyo vilianzia China, vimesambaa katika nchi mbalimbali duniani na kusababisha mamia a watu kuathirika na wengine kufariki dunia.

# Toke huiamini serikali yako kwenye corona



STAA`wa Nigeria, Toke Makinwa, anaamini serikali haina idadi kamili ya watu walioambikizwa ugonjwa wa corona.

Kwa hivi sasa dunia imetaharuki kutokana na ugonjwa huo kusambaa kwa kasi na kuathiri watu wengi.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, Makinwa, amesema hawezi kuamini kwamba serikali ina idadi kamili ya watu walioathirika kitu ambacho ni hatari.

"Tunaendelea na kuamini kwamba hakuna watu wengi waliopata virusi vya corona nchini Nigeria? Sifikirii kama idadi iliyotolewa ni kweli , jamani waokoeni hao watu," amesema Makinwa.



## Pole Oprah kumbuka ukubwa jalala

MTANGAZAJI na mtayarishaji maarufu wa kipindi cha mazungumzo nchini Marekani, Oprah Winfrey, amekana uvumi kwamba anashikiliwa na polisi kutokana na kesi ya kumgonga mtoto kwa gari.

Oprah aliandika katika ukurasa wake wa Twitter kwamba suala hilo sio kweli na kwamba mtu aliyezusha jambo hilo ana lengo la kumchafulia jina.

"Kuna taarifa zimesambaa kwenye mitandao kupitia simu zenu, jaribuni kuzipuuza kuwa habari hizo za kubuni kwamba eti nimekamatwa, siyo kweli nipo salama," amesema.

## Wengi wamsikitikia Elba kupata corona

TAARIFA za kupata maambukizi ya virusi vya corona kwa nyota wa uigizaji wa Uingereza, Idris Elba, imewashtua watu wengi.

Msanii huyo alitangaza kupata ugonjwa huyo kupitia video fupi aliyeposti kwenye ukurasa wake wa Twitter , ambapo amesema vipimo vinaonyesha amepata maambukizi ya corona

Idris amesema kwa sasa hana dalili zozote za ugonjwa huo na kwamba aliupata baada ya kukutana ana mtu ambaye alikuwa na ugonjwa huo.

Baada ya kujua tatizo hilo amejiweka mbali na mkewe Sabrina ili kumlinda.





## Duh! Keri huo utafiti wako umekwenda mbali

MWANAMUZIKI wa Marekani, Keri Hilson, amekuwa na maoni tofauti kuhusu chimbuko la virusi vya corona ambavyo kwa sasa vinatikisa dunia.

Keri amesema virusi hivyo vinaweza kusababishwa na matumizi ya mionzi ya kieletroniki na sio wanyama kama inavyodaiwa.

"Tuwe wakweli, nasema kuna uchunguzi mwingi inaonyesha uhalisi kuna uwezekano kuwa ni kiwango cha juu cha mionzi ya kieletroniki inachangia," ameandika Keri kupitia akaunti yake ya Twitter

## Gift wewe huna uzalendo?

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Nigeria, Gift Powers, amechafua hali ya hewa baada ya kueleza kwamba Ghana ndio nchi pekee inayoongoza kiuchumi kuliko Nigeria.

"Ghana ndiyo ingeitwa nchi inayoongoza na si Nigeria" amesema Gift.

Gift ambaye ni raia wa Nigeria, amesimamia kauli yake kwa kueleza haiingii akilini Ghana ambayo inaongoza kwa kila sekta kuwa chini ya Nigeria ambayo kimsingi hakuna maendeleo ya kutosha.



## MAKALA



**KALAMU YA MWALIMU**

# Hofu na kutojiamini adui wa wanawake-2

**Na Reubeni Lumbagala**

JUMA lililopita, ilikuwa sehemu ya kwanza ya makala haya. Kutokana na umuhimu wake na maoni ya wasomaji wangu, nimeona ni vyema kuuendeleza mjadala huu muhimu kwa ustawi na maendeleo ya nchi yetu kupitia mchango wa wanawake.

Katika makala iliyopita, nilieleza namna ambavyo wanawake ni kundi muhimu katika maendeleo, kuanzia ngazi ya familia, jamii hadi taifa. Kupitia mchango wa wanawake, jamii nyingi zimepiga hatua za kimaendeleo na zinaendelea kufanikiwa hasa pale wanawake wanaposhirikishwa kikamilifu kama watu muhimu kwenye kutekeleza mipango na majukumu mbalimbali.

Tatizo kubwa linalowakabili wanawake wengi katika jitihada za ukombozi na maendeleo yao kwa ujumla huenda ni hofu na kutojiamini. Hofu na kutojiamini imekuwa ni tatizo ambalo kama wanawake wenyewe hawatajizatiti kukabiliana nalo, mipango na juhudi zao nyingi zitakwama na hivyo kubaki nyuma huku wanaume wakiendelea kujiimarisha zaidi kwenye kila eneo la maendeleo.

Wanawake wanapaswa kujiamini kuwa wanao uwezo wa kufanya mambo makubwa katika jamii. Mwanamke akijiaminisha kuwa uwezo binafsi alionao unaweza kumfanikisha katika mipango yake, hofu na kutojiamini havitakuwepo kwake. Ni muhimu kwa wanawake kuwa na ndoto kubwa na waamini kuwa wanao uwezo binafsi bila msaada wa mtu mwingine kumfanikisha.

**MADHARA KUTOJIAMINI**

Mosi, hofu na kutojiamini kunazuia uthubutu wa wanawake. Uthubutu ni nyenzo muhimu ya mafanikio. Anayethubutu ni yule ambaye tayari ameshinda hofu na ameamua liwalo na liwe hadi afanikishe kile alichokusudia kukifanya. Adui hofu na kutojiamini ni kikwazo cha uthubutu, hivyo kuendeleza hofu ni kuzuia uthubutu, ni kuzuia maendeleo.

Kwa kuishinda hofu na kutojiamini, kunajenga uthubutu na uimara wa wanawake kuwa nao wanao uwezo wa kufanya mambo makubwa ya kimaendeleo, na kugeuza imani potofu waliyonayo baadhi ya wanajamii kuhusu uwezo wa wanawake.

Pili, hofu na kutojiamini kunamfanya mwanamke abaki kuwa mtazamaji na juhudi za kimaendeleo zinazofanywa bila kuchangia chochote. Mwanamke ni muhimu katika kufanikisha malengo, mipango, dira za maendeleo. Ndiyo maana hata nembo ya Tanzania, kuna picha ya mwanamume na mwanamke kuonyesha umuhimu wa jinsi zote mbili katika maendeleo ya taifa. Kwa kuwa wanawake wanategemewa kwa maendeleo ya nchi ni vyema wakawa jasiri na kujiamini kuwa wanaweza, ili washiriki kutoa mchango wao wa kimaendeleo.

Tatu, kuongezeka mahitaji ya uwepo wa semina, makongamano na warsha mbalimbali za kuwajengea uwezo wanawake. Uendeshaji wa semina na makongamano yanagharimu fedha nyingi hadi kukamilika kwake. Semina zinatumika kuwaelimisha watu katika jamii wakiwemo wanawake. Mahitaji ya uwepo wa semina na makongamano ya mara kwa mara kwa ajili ya wanawake yanaweza kuongezeka maradufu kwa ajili ya kupambana na adui hofu na kutojiamini. Hii itasababisha uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha ili mkufanikisha semina za wanawake ili kuwajengea uwezo ili nao wajiamini. Hivyo, upo uwezekano wa kuokoa fedha nyingi za semina za kuwajengea uwezo wanawake kama juhudi za kushinda hofu na kutojiamini zitazaa matunda.

Nne, wanawake wataendelea kubaki nyuma na daima watahitaji msaada wa wanaume kama msingi wa ukombozi wao. Msingi na mkombozi wa wanawake ni wanawake wenyewe, hivyo kuendelea kuwa na hofu na kutojiamini, ni kuwatishwa mzigo wanaume wa kuwasaidia kuwakomboa ili hali ufunguo wa ukombozi wanao wanawake wenyewe kwa kubadili fikra, kujiamini, kuwa na uthubutu na kushinda hofu.

Pamoja na utayari wa wanaume kuwasaidia wanawake, lakini wanaume hawapaswi kuwa msingi wa ukombozi wa wanawake. Ni wajibu wa wanawake wenyewe kuhakikisha kuwa hawabaki nyuma kushiriki kwenye ukombozi wao wenye tija kwao wenyewe, familia zao, jamii na Tanzania.

Tano, wanawake kushindwa kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi. Katika ulingo wa siasa, wanahitajika sana kwani nao wana uwezo mkubwa wa kuongoza na kutumikia nafasi mbalimbali za uongozi. Hofu na kutojiamini kunazuia wanawake kushindwa kujitokeza kwa wingi kuwania uongozi kwa kuhofia kuwa hawana uwezo wa kuongoza.

Hata nafasi za uteuzi zitakapotokea, wanawake watashindwa kupata nafasi hizo kwani hawatakuwa tayari kupewa majukumu hayo kwa kujaa hofu. Ili kuepusha kukwamisha juhudi za kuwashawishi wanawake kugombea nafasi za uongozi, adui hofu na kutojiamini ni lazima atokomezwe.

Kwahiyo, katika mipango mingi inayofanywa na serikali na asasi mbalimbali za kiraia katika kuwainua wanawake, ni lazima mkazo uwepo wa kushughulikia tatizo la hofu na kutojiamini walilonalo baadhi ya wasichana na wanawake. Mchango wa wanawake unahitajika sana katika nchi yetu ili kufanikisha juhudi za maendeleo. Katika hatua mbalimbali za maendeleo, wanawake washirikishwe kikamilifu ili kupata maoni na ushauri wao, Wanawake msijidharau, mnaweza, msirudi nyumba, songeni mbele.

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

# Virusi vinavyotikisa dunia zama hizi

**Na Mwandishi Wetu**

KWA kipindi cha miaka 30 iliyopita idadi ya milipuko ya virusi imeongezeka, na magonjwa yamesambaa kwa kasi kama ilivyo kwa virusi vya corona nchini China hivi sasa vimeendelea kusambaa dunia nzima.

Ni ukweli kuwa hivi sasa idadi ya watu imekuwa kubwa kuliko nyakati zote zilizowahi kutokea - Idadi ya watu duniani kwa sasa ni zaidi ya bilioni 7.7 China na India zikiongoza kwua na watu wengi zaidi.

Watu wengi zaidi wanaoishi katika maeneo yenye nafasi ndogo inamaanisha kuwa kuna kuwa na hatari zaidi ya kupatwa na wadudu wanaosababisha ugonjwa na pia maradhi kusambaa kwa kasi zaidi.

Virusi vya corona ndivyo vinavyotikisa dunia sasa na vinaelezwa kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya. Kugusa maji maji za mwili kama makamasi.

Virusi huishi kwa muda fulani nje ya mwili, hivyo kwa kuwa karibu ugonjwa huenea.

Mwaka 2014 ugonjwa ulisambaa kwa kupitia damu na maji maji mengine, lakini kwa wale wanaokuwa karibukaribu wanaweza kuambukizana.

Lakini si virusi vyote huambukizwa kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Duniani leo kuna uwezekano wa kusafiri kwa siku moja kutoka bara moja kwenda jingine virusi vya mafua vinaweza kusambaa haraka mno

**ZIKA**

Mathalani zika, ambayo huambukizwa kutoka kwa mbu kwenda kwa mwanadamu. Mbu wanaosababisha zika huishi katika maeneo ya mijini ambao huzaliana kwenye maeneo yenye watu wengi, unyevunyevu na maeneo ya joto.

Homa ya Zika husababishwa na virusi vya Zika, jamii ya jenasi Flavivirus. Dalili zake zinafanana na zile za virusi vingine vya jenasi hiyo, kama vile Homa ya dengue au ya chikungunya.

Homa hizo humshambulia mtu kwa na kudumu kwa siku kati ya nne na saba. Asilimia kubwa 60 hadi -80 homa hizo hazina dalili za pekee.

Wagonjwa wenye dalili wana homa kidogo, maumivu ya muda kwenye viungo hasa mikononi na miguuni) na kuwashwa ambao mara nyingi huanzia usoni na kuenea katika sehemu zote mwilini.

Pamoja na kwamba ugonjwa huo hauna dalili za kutisha, wataalamu wa afya wanauhusisha na tatizo la kuharibu mimba za na kusababisha kuzaliwa watoto wenye ulemavu.

Mara ya kwanza na mlipuko uliripotiwa mwaka 2015 nchini Brazil ambao mwaka 2016 ulizidi kuenea barani Amerika.



Mtoto ameathirika na virusi vya zika baada ya mbu wanaoeneza kirusi hicho kumshambulia mama yake wakati wa ujauzito. **PICHA:MTANDAO.**

**NIPAH**

Ni ugonjwa wa virusi ambao ni hatari unaoenezwa na popo ukidaiwa kuanzia na kuua watu tisa nchini India mwaka juzi.

Maofisa wa afya katika jimbo la Kerala, kusini mwa India walithibitisha kwamba watu tisa walifariki kutokana na kinachodhaniwa kuwa virusi hatari vya Nipah.

Nipah ni ugonjwa ambao unaweza kuambukiwa binadamu kutoka kwa wanyama.Hakuna chanjo yoyote ya ugonjwa huo kwa sasa na asilimia 70 ya wanaoambukizwa virusi hivyo hufariki dunia.

**EBOLA**

Ebola ni ugonjwa unaosabibishwa na virusi vya homa ya hemoraji "kuvuja damu sana". Ina kiwango cha juu cha uambukizaji; watu wengi wanaombukizwa haraka na hufariki.

Huo ugonjwa wa damu kutoganda na unaua sana kwani kati ya watu 10 waliopata virusi vya Ebola, wastani kati ya watano hadi tisa hufa. Ebola haina chanjo wala tiba lakini kupokea matibabu katika vituo vya ebola mapema huongeza uwezekano wa kupona.

Kwa ujumla magonjwa ya virusi kama ebola, mafua ya ndege yaliyotokana na virusi vya SARS na sasa virusi vya corona vyote ni virusi vinavyoambukizwa kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu, virusi vya corona vimeanzia kwenye soko la nyama mjini Wuhan nchini China japo ripoti za awali zinasema inaweza kuwa kutoka kwa nyoka. Kwa upande wa ebola vinadaiwa vilitoka kwenye ulaji wa nyama za sokwemtu .

**Na Mtandao**

# FANYA HAYA UEPUKE TATIZO

## ■Misosi: Zingatia dona zaidi,

**Na Mwandishi Wetu**

KUKIMBILIA kwa waganga wa kienyeji wanaojiita wabobezi wa kuimarisha afya ya uzazi ili kubeba mimba na kuongeza nguvu za kujamiiana ni jambo unaloweza kuliepuka kwa kula milo inavyoimarisha mfumo wa uzazi na si kuchanjwa wala kubebeshwa mizigo ya miti dawa.

Vyakula vitakavyosaidia mfumo wa uzazi kuimarika na kufanikisha upevushwaji wa mayai na kuboresha nafasi ya kushika mimba, tena kujifungua mtoto mwenye afya na salama ndiyo mambo ya kuzingatia badala ya kupigwa chale mwili mzima na hata kubakwa na waganga wa kienyeji kwa kisingizio cha kupata ujauzito.

Hilo linawahusu kinamama na kwa upande wa wanaume ni muhimu kwao kutumia vyakula vyenye virutubisho muhimu ili kuimarisha mfumo wa uzazi.

Wanashauri kula vyakula vyenye 'beta-carotene' ambavyo ni karoti, viazi vitamu, mboga za kijani -spinachi, figiri, majani ya maboga, letusi, pilipili hoho za njano na kijani.

Zote hizo huimarisha homoni na kuboresha uwezo wa mwanamume kushiriki tendo la kujamiiana na mama kupata ujauzito.

VITAMIN B

Ni muhimu kutumia vitamin B, inayopatikana kwenye dona kama mkate wa brown, ugali wa dona, mchele wa 'brawn' mtama , mwekundu na shayiri. Nyama imo hasa ya ng'ombe, kuku, samaki, mayai, maziwa jibini, maharage jamii zote kuanzia kunde, choroko njugu mawe na dengu.



Vyakula vyenye beta carotene kama karoti, viazi vitamu na maboga vinahusika na kuleta hali bora ya viungo vya uzazi.



Spinachi jamii ya kale ni muhimu ina vitamin C ya kutosha inayoimarisha afya ya uzazi kwa wanawake na wanaume.

Kwa taarifa yako vitamini hii ipo kwa wingi kwenye mbegu za mafuta kama alizeti, karanga, kweme, spinachi na matunda jamii ya machungwa, maparachichi na ndizi.

Vitamini hii husaidia mfuko wa mayai wa mwanamke wakati wa kupevushwa yai kuwa imara na pia huepusha mimba kuharibika.

Ni muhimu kutumia vyakula vyenye foliki asidi kumuepusha mtoto na matatizo ya neva za fahamu kwa kuzaliwa na mgongo wazi na kichwa kikubwa.

**VITAMINI C**

Unavipata ukila koliflowa, spinachi jamii ya kale, juisi ya machungwa, papai, pilipili hoho za kijani, njano au nyekundu viazi vitamu na nyanya. Vitamini C inasaidia kufyonza homoni ya pogesteroni.

**VITAMIN D**

Imesheheni kwenye vyakula kama mafuta ya samaki, jodari, vibua, maziwa mgando, juisi zikiwamo za machungwa, mayai na maini.

Mlo wenye vitamin D husaidia kuboresha uwezo wa kupata watoto kwa wote wanawake kwa wanaume. Aidha, inatibu matatizo ya uzazi kama uvimbe kwenye mfuko uzazi, kwenye mfuko wa mayai, na kuboresha mbegu za kiume kwa kuzifanya imara.

**VITAMIN E**

Afya ya uzazi huimarika kwa kula vyakula vyenye vitamin E iliyomo kwenye mafuta ya mbegu kama ya nazi, karanga, ufuta, soya, karanga, almond na njugu mawe na jamii ya siagi.

Vyakula hivi hukuza afya ya yai kwa kinamama na mbegu za kiume kwa wanadamu.

**MADINI CHUMA**

Vyakula hivi ambavyo ni pamoja na maini, kuku, nyama ya kondoo, dagaa, nyama nyekundu, mayai na nyama ya bata ni muhimu kwani vimesheheni madini ya chuma yanapunguza nafasi za ugumba unaosababishwa na mayai kushindwa kupevushwa kwa upande wa wanawake.

Vitamini jamii ya Omega 3 na asidi za mafuta zinasidia kuboresha idadi ya mbegu za kiume na

MAKALA

# Fanya haya kuepuka tatizo ugumba, nguvu za kiume

INATOKA UK. 22

kwa upande wa wanawake.

Vitamini jamii ya Omega 3 na asidi za mafuta zinasidia kuboresha idadi ya mbegu za kiume na uwezo wake wa kutembea kutoka sehemu moja kwenda nyingine vilevile na kuongeza kasi ya damu kwenye mfuko wa uzazi.

Omega 3 hupatikana kwa wingi kwenye samaki, karanga zenye ganda gumu, samaki jamii ya jodari na mboga hasa spinachi na kale.

**VIONDOA SUMU**

Kitaalamu huitwa 'antioxidants' vina kinga na kutibu ugumba. Viko kwenye mboga kama kale -jamii ya spinachi, kabeji nyekundu, maharage na bitiruti. Madini ya zinki pia yanaimarisha ubora wa mbegu za kiume.

Aidha, kutumia vyakula vyenye mafuta mengi vinaweza punguza hatari za ugumba unaosababishwa na yai kushindwa kupevushwa.

**KUJIONGEZA**

Wakati mwingine si lazima kufikiria kuwa unapaswa kupata vyakula kwa bei mbaya cha msingi ni kutumia kile kilichopo kwenye mazingira yako kwa mfano. Vyakula vinavyoweza kuongezwa kwenye mlo wa kila siku ni pamoja na mboga za majani kama spinachi hizi zina utajiri wa vitamini C na foliki asidi.

Pia zinasaidia kuboresha upevushwaji wa yai, utengenezaji wa mbegu za kiume ulio bora na mzuri na kupunguza nafasi ya mimba kuharibika au magonjwa ya kurithi.

Brocoli zina wingi wa vitamin C ambayo ni muhimu kwenye upevushwaji wa yai. Kabichi ni mboga nzuri kwa wanawake wenye matatizo ya uzazi. Pia ni chanzo kizuri cha 'Di-indole methane,'inayosaidia kumkinga mama na uvimbe wa mfumo wa uzazi na endometriosis.

Unaweza kuongeza viazi kwa sababu vina wingi wa vitamin C na hutibu kasoro za masuala mengi ya uzazi hasa kwa wanawake.

Ni muhimu sana kutumia nyanya kwa wanaume kwani zina wingi wa 'lycopene,' inayosaidia kuboresha idadi ya mbegu za kiume na kuongeza kasi ya mbegu kuogelea. Lakini pia hudhibiti madhara yanayotokana na kumizwa kwa seli.

Ni vyema kula karoti mara kwa mara kwani ni chanzo kizuri cha beta-carotene, aidha ulaji wa viazi vikuu nao ni muhimu kwani una phytoestrogens, ambazo zinahamasisha utoaji wa yai kutoka kwenye mfuko wa mayai na kusaidia kutibu kasoro za mbalimbali kwenye mfuko wa uzazi kwa wanawake.

**MATUNDA**

Matunda ni chanzo kizuri cha antioxidants, ambazo ni muhimu katika uzazi na afya kwa ujumla. Kwa mfano unaweza kula komamanga ni chanzo kizuri cha vitamini C, na inasaidia kuongeza hamu ya kufanya tendo la ndoa.

Parachichi hili ni muhimu kwa wanandoa, wanawake wanaotafuta watoto na kila mmoja anayetaka kuwa na afya bora ya kizazi.

Lina wingi wa vitamin B ambayo ni muhimu katika ukuaji wa seli na mfumo wa uzazi, vitamin E na pia lina nyuzinyuzi au fibres zinazosaidia kulainisha chakula tumboni, madini na mafuta muhimu. Vitamin E inasaidia kutunza ukuta wa mfuko wa uzazi na kupunguza uwezekano wa kizazi kulegea.

Ndizi mbivu ni muhimu ina wingi wa vitamin B6 na potasiamu na inasaidia kuboresha uwezo wa kupata ujauzito kwa kusimamia homoni na kuimarisha ubora wa yai na mbegu za kiume.

Kutumia zabibu na machungwa matunda yanayosaidia kuboresha afya ya yai kwasababu ya wingi wa virutubisha vya "polyamine putrescine" ndani yake.

Mananasi yamejaa vitamin C inayosaidia kukuza na kuongeza nafasi ya kupata ujauzito kwa mwanaume na kupunguza hatari ya uvimbe kwenye mfuko wa mayai na kwenye ovari. Nanasi linakuza ubora wa mbegu za kiume kwa wanaume wanaovuta sigara.

Vyakula visivyo mbogamboga kama nyama, samaki, na mayai ambavyo vina wingi wa omega3-fati aside ni muhimu.

Kwa upande wa mayai yana wingi wa omega-3, foliki asidi na vitamin D. Nyama ya kuku au ya ng'ombe , mbuzi na ni chanzo kikubwa cha madini ya chuma na mafuta muhimu.

**MAZIWA**

Kumbuka yana wingi wa madini ya kalshamu, mafuta na vitamin D bidhaa zitokanazo na maziwa ni muhimu katika kuimarisha uwezo wa kupata ujauzito kwa wanandoa ambao wanataka kuwa na watoto haraka. Maziwa yana wingi wa kalsiamu na mafuta, mtindi ni chanzo kizuri cha kalsiamu na vitamin D.

**VIUNGO**

Hii inasaidia kuendeleza usawa wa homoni ya estrojeni kwa mwanake na kuimarisha uwezo wa kupata ujauzito.

Tumia binzari ina wingi wa antioxidants na inasaidia kutibu matatizo yote yanayohusiana na hedhi wakati kitunguu saumu kinakuza uwezo wa kushika mimba na kina antioxidant inayosaidia mbegu za kiume kusafiri kwa haraka na kuongeza nafasi ya kupata ujauzito ikiwa utatumia siku tano zote za kupevushwa yai.

**MAFUTA, MBEGU**

Mbali na mboga, matunda na nyama mbegu na mafuta yake yanachukua jukumu kubwa katika kuboresha nafasi ya kushika mimba. Baadhi ya mafuta hayo ni kama:

Mafuta ya (mizeituni) olive, yanatoa mafuta yaliyo muhimu katika mwili yanayosaidia kupunguza kuvimba mwili kwa ndani na kuongeza umakini wa insulini ndani ya mwili wa kinamama.

Inaboresha nafasi ya kupata ujauzito kwa wanawake waliopandikiza watoto, mbegu za maboga zinasifika kwani zina wingi wa zinki ambayo inasaidia kusimamia afya ya mfumo wa uzazi.

Pia zinki inasaidia kuongeza viwango vya homoni ya testosteroni na mbegu za kiume na kuimarisha mtiririko wa damu kwenye viungo vya kiume vya wanaume na mfumo wa uzazi. Tena inahusika na kuzalisha mayai yaliyokomaa, utaipata kwa kula mbegu za alizeti.

**MBEGU KAVU**

Kwa mfano almond zina wingi wa vitamin E na omega-3 asidi, karanga nazo zina a wingi wa omega-3 , madini ya magnesiamu na nyuzinyuzi zinazosaidia mmeng'enyo wa chakula tumboni na kukuwezesha kupata choo laini. Pia madini haya huboresha nguvu za manii na kasi yake pia.

**JAMII MIKUNDE**

Kunde na maharage yana utajiri wa protini, nyuzinyuzi na vitamin B. Nafaka kama mchele, ngano, mtama isiyokobolewa ni kuwa myeupe ni muhimu kwa kuwa zina wingi wa nyuzinyuzi na husimamia kiwango cha sukari, hivyo kuendeleza kiwango cha foliki asidi ili kusaidia kumwekeza mwanamke kwenye nafasi ya kupata ujauzito.

**VYA KUEPUKA**

Mara nyingi wanawake wanakuwa na matatizo ya kupata ujauzito kutokana na kutumia jamii za vyakula vyenye sumu mfano vyenye mabaki ya dawa za viwandani za kukuza mazao.

Ni vyema kuepuka vyakula viliyowekewa dawa za kuua wadudu kwenye mboga za majani, pilipili, au zabibu dawa zina athari zinapunguza nafasi ya kupata ujauzito.

Vyakula vya baharini kama samaki wa maji chumvi, walio na zebaki nyingi huleta ugumba. Zebaki zinazotumiwa kwa wingi maeneo ya kuchenjua dhahabu nayo ni hatari kwa afya huleta ugumba na kuharibika mimba.

Pia epuka vyakula vinavyokaangwa kwenye mafuta kama chips, viazi , samaki wa kukaanga si salama sana iwapo unataka kupata ujauzito.

Vyakula vyenye wanga kidogo vinaweza kuongeza ugumba kwa kuhatarisha viwango vya insulini mwilini kuwa chini, lakini pia vyakula vyenye sukari na nafaka zilizokobolewa zinaweza kuongeza kiwango cha sukari kwenye damu na kusababisha ugumba unaosababishwa na yai kushindwa kupevushwa.

**Makala hii imetoka Afya Track.**



Nafaka (dona) zisizokobolewa kuanzia mkate, ugali wa dona, uji wa mtama ni muhimu si kwa kuimarisha michakato ya uzazi pekee bali pia kulinda afya ya mfumo wa chakula na kuweka mizania ya insulin. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Uwekezaji usiozingatia haki ni balaa kwa nchi

Na Sabato Kasika

MIGOGORO ya ardhi nchini ni kero inayojitokeza mara kwa mara katika jamii kuanzia kaskazini hadi kusini tena ikiwa na viwango tofauti, kwani kuna mingine iliyosababisha uhasama, uharibifu wa vitega uchumi na hata mauaji.

Uhasama na migogoro hiyo huibuka kati ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi wakiwamo wakulima, wafugaji, wawekezaji wakigeni na wazawa na wachimba madini huku ikisababisha athari nyingi na mbaya miongoni mwa wahusika.

Pamoja na athari hizo , juhudi zinafanyika kumekuwapo na msukumo wa kijamii wa kukubaliana na migogoro ya ardhi kila inapotokea, lengo likiwa ni kuepusha au kudhibiti utokeaji na athari zinazoweza kusababishwa na migogoro hiyo.



Wadau wakifuatilia mkutano uliojadili uwekezaji unaozingatia haki za binadamu.

Kuna mikoa mbalimbali ambayo imeshuhudia migogoro ya ardhi ukiwamo wa Morogoro, Pwani na Mbeya kwenye mashamba ya mpunga na kusababisha chuki miongoni mwa wananchi wenyewe na hata kwa wawekezaji.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wadau wa biashara na haki za binadamu wanatoa ushauri ambao wanaamini kwamba unaweza kusaidia kuepusha migogoro na pia kulinda haki za binadamu.

Wadau ambao hivi karibuni walikutana katika mkutano wa mwaka jijini Dar es Salaam, na kuonyesha kufurahia jinsia Tanzania inavyopambana na migogoro hiyo.

Aidha, wanasema, ni muhimu kuzingatia uwekezaji wenye manufaa kwa taifa na kuwe na uhakika kwamba haki za binadamu zinalindwa ili kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza.

Hilo linatajwa katika mkutano huo uliojadili uwekezaji unaozingatia haki za binadamu, kuwa kadri shughuli za biashara zinavyopanuka katika sekta binafsi, athari chanya na hasi kwenye jamii huongezeka.

Na kwamba mashirika ya kimataifa yanaweza kuchangia katika uchumi na ajira na kuleta furaha na haki za binadamu na pia yanaweza kuleta athari upande wa haki za binadamu wakati wa utendaji kazi, hivyo kampuni zina wajibu wa kuheshimu haki za binadamu.

## UWEKEZAJI WA HAKI

Wakili Flaviana Charles ni Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BRHT), ambaye anawaambia wadau kwenye mkutano huo kuwa kuna uhusiano kati ya biashara na haki za binadamu.

Anasema uwekezaji mwingine unaweza kusababisha uchufuzi au uharibu wa mazingira hali ambayo ni ukiukwaji wa haki za binadamu, hivyo ni muhimu tathmini ifanyike kabla ya uwekezaji.

"Kuna uhusiano mkubwa kati ya biashara na haki za binadamu, ndiyo maana tunasisitiza kuwa na uwekezaji unaozingati hilo, na ushirikishwaji wa wananchi wa maeneo husika ni muhimu," anasema Flaviana. Anasema, tangu mwaka 2017 asasi yake kwa kushirkiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) na Shirika la IPIS kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), inafanya uboreshaji wa ufuatiliaji, utafiti na mazungumzo juu ya biashara na haki za binadamu Tanzania.

"Umoja huo una kitengo chake cha Demokrasia na Haki za Binadamu (EIDHR), ambapo tumebaini mambo mengi kwenye uwekezaji yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho ili uwe unaozingatia haki za binadamu," anasema.



Mshauri wa Jumuiko la Maliasili Tanzania, Daniel Ouma, akitoa maoni yake.
**PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

## MAFUNZO VIJIJINI

Mkurugenzi Mtendaji wa Haki Ardhi, Cathbert Tomitho, anataka viongozi wa vijiji wajengewe uwezo wa kuzijua sheria ili waepuke kushawishiwa na wawekezaji wasiozingatia haki za binadamu.

"Lakini pia wanasiasa wanachangia kuwapo kwa sintofahamu hiyo kwa kuwaagiza viongozi wa vijiji kutoa ardhi kwa wawekezaji, hii inatokana ukweli kwamba wengi hawajui sheria ndiyo maana wanakubali," anasema Tomitho.

Anasema, njia pekee ni viongozi hao wa vijiji na wajumbe kupewa elimu ya kuhusu sheria mbalimbali zikiwamo za ardhi ili waepuka kuingizwa katika mtego na wanasiasa na kuleta migogoro au uvunjifu wa haki za binadamu.

Tomitho anasema, ushiriki wa wananchi katika mchakato wa utwaaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji ni muhimu, hivyo waelimishwe ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu haki za ardhi na uwekezaji, kwa vile ni wadau wakubwa kwenye mchakato wa utwaaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

"Utwaaji wa ardhi usio wa haki na fidia isiyostahili, vinaweza kusababisha uvunjifu wa haki za binadamu, ikiwamo haki ya afya, haki ya kumiliki mali, haki ya kufaidika na maliasili na haki ya mazingira safi na salama," anasema.

## MIGOGORO ISIYOISHA

Mkurugenzi wa Hakiadhi, Timotho, anakumbusha kuwa utwaaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji usiozingatia haki, unachangia kuwapo kwa migogoro ya ardhi, ikiwamo ya wanakijiji na wawekezaji, wakulima na wafugaji.

Anasema, wakati mwingine baadhi ya vyanzo vya msingi vya migogoro kati ya wawekezaji na wananchi huwa ni wawekezaji kutoa ahadi za uongo kwa wananchi ili kuwawezesha kupata ardhi lakini hawazitekelezi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BRHT), Wakili Flaviana Charles, akizungumza kwenye kwenye mkutano huo.

"Mwekezaji anaweza kuahidi kutoa ajira, kuboresha miundombinu mbalimbali, kufanya tathmini ya athari za kimazingira, kutoa huduma za jamii ikiwamo elimu, afya na maji, lakini mwisho wa siku hayo hayafanyiki," anasema.

## CHANZO WANANCHI?

Kwa upande wake Mkurugenzi wa asasi ya Maendeleo ya Jamii ya Mabadiliko ya Kiafrika, Jackson Muro, anawatupia lawama baadhi ya wananchi kwamba wanachangia kuwapo kwa tatizo hilo.

Anasema, uelewa mdogo juu ya haki zao unasababisha wasihudhurie vikao vya ngazi za vijiji kwa ajili ya mambo ya ardhi na mazingira, jambo ambalo kwa namna moja ama nyingine linasababisha changamoto hizo.

"Vilevile wapo baadhi ya viongozi wasioitisha mikutano ya vijiji kutokana na sababu wanazozijua wenyewe, lakini kikubwa zaidi ni kukwepa kuulizwa maswali na wananchi kama kuna jambo wamefanya vibaya," anasema Muro.

Anakumbusha kuwa biashara inayozingatia haki za binadamu itafanikiwa iwapo kutakuwa na ushirikishwaji, kuanzia kwa mwekezaji, viongozi wa serikali na wananchi, na kwamba mmojawapo akiwekwa kando ni tatizo.

Mshauri wa Jumuiko la Maliasi Tanzania, Daniel Ouma, anataka wafugaji kupunguza wingi wa mifugo kwa ajili ya kuepusha uharibifu wa mazingira na hatimaye kuwa na biashara yenye tija.

Ouma anasema, mabadiliko ya tabianchi yamechangia mambo mengi, lakini pia watu wanaongezeka, lakini ardhi ni ileile, hivyo ipo haja ya kuzingatia matumizi ya ardhi kulingana na mabadiliko hayo.

"Kwa wafugaji ni kupunguza wingi wa mifugo, na hatua hiyo itaepusha kuhama mara kwa mara hali ambayo imekuwa ikichangia uharibifu wa mazao ya wakulima na migogoro ya ardhi," anasema Ouma.

# Wanne wanyongwa kwa kubaka na kuua

**NEW DELHI, India**

WANAUME wanne raia wa India waliofungwa kwa kumbaka na kumuua mwanafunzi mjini Delhi mwaka 2012 wamenyongwa.

Wanne hao ni Akshay Thakur, Vinay Sharma, Pawan Gupta na Mukesh Singh ambao walihukumiwa kifo mwaka 2013 walinyongwa katika Gereza Kuu la Tihar ikiwa ni mara ya kwanza hukumu ya kifo kutekelezwa India kutoka mwaka 2015.

Muathiriwa alifariki kutokana na majeraha aliyopata siku kadhaa baada ya kubakwa na wanaume sita ndani ya basi.

Kisa hicho kilizua ghadhabu ya umma ambayo ilichangia kuandikwa kwa sheria mpya dhidi ya ubakaji nchini India.

Mwanafunzi huyo wa miaka 23 aliyepewa jina la Nirbhaya na vyombo vya habari kuashiria mjasiri, hakuweza kutajwa jina lake halisi kwa mujibu wa sheria za India.

Watu sita walikamatwa kwa kumshambulia ambapo mmoja wao, Ram Singh, alipatikana akiwa amefariki ndani ya jela mwezi Machi mwaka 2013, katika kile kinasadikiwa kuwa alijiua.

Mwingine aliyekuwa na miaka 17 wakati wa shambulio hilo, aliachiliwa huru mwaka 2015 baada ya kufungwa kwa miaka mitatu katika kituo cha kurekebisha tabia muda ambao ni wa mwisho kumfunga mtoto nchini humo.

Katika miezi ya hivi karibuni, wafungwa wote wanne waliwasilisha ombi katika mahakama ya juu zaidi ikiwa ni juhudi ya kutaka hukumu yao ibadilishwe kutoka kifo hadi kifungo cha maisha gerezani.

Lakini, ombi lao lilikataliwa, hatua ambayo iliwaacha bila njia nyingine ya kisheria ya kujinusuru.

Rufaa ya mwisho ya kutaka hukumu ya kifo isitekelezwe dhidi yao pia ilikataliwa saa kadhaa kabla ya wote wanne kunyongwa.

Dakika kadhaa baada ya wafungwa hao kunyongwa Ijumaa asubuhi, mama yake muathiriwa alisema, "Nilitundika picha ya binti yangu ukutani na kumwambia hatimaye tumepata haki."

Baba yake alisema, "Mahakama imerejesha hadhi yake".

Kundi la watu waliokuwa wamekusanyika nje ya lango la gereza hilo wakiwa wamebeba mabango walianza kushereheka baada ya tangazo la kunyongwa kwa wafungwa hao wanne kutolewa.

Baadhi ya waliimba "kifo kwa wabakaji" na huku wakishukuru idara ya mahakama kwa hatua hiyo.

Mwanafunzi huo aliyebakwa kisha kuawa Desemba 16 mwaka 2012 alipanda basi saa 2:30 usiku akiwa na rafiki wa kiume.

Walikuwa wanarejea nyumbani baada ya kutizama filamu katika ukumbi wa sinema.

Wanaume sita ambao walikuwa ndani ya basi hilo, waliwashambulia na kisha kumbaka kwa zamu mwanamke huyo na baadaye kumpiga kwa kutumia kifaa butu ambapo tukio hilo la kupigwa lilimtokea pia rafiki yake aliyekuwa naye.

Baada ya hapo watuhumiwa hao waliwarusha nje ya basi na kuaachwa wafe.

Wapita njia waliwakuta waathiriwa wakiwa uchi na nyuso zilizojaa damu kisha walijulisha polisi ambapo wiki mbili mbele yalifanyika maandamano ya umma ya kushinikiza India kuingilia kati jinsi inavyoshughulikia masuala ya wanawake.

Muathiriwa alifariki katika hospitali moja nchini Singapore, ambako alipelekwa kwa matibabu baada ya hali yake kuzorota katika hospitali ya Delhi.

**BBC**




Govana Gavin Newsom, anasema zaidi ya watu milioni 40 katika jimbo lake wanaweza kupata maambukizi ya virusi vya Covid-19 katika miezi miwili ijayo. PICHA:MTANDAO

# Mkutano wa kilele wa G7 wafutwa sababu corona

**WASHINGTON, Marekani**

SERIKALI ya Marekani imefuta mkutano wa ana kwa ana wa kilele wa wakuu wa kundi la mataifa yaliostawi zaidi kiviwanda duniani (G7).

Mkutano huo ulipangwa kufanyika mwezi Juni mwaka huu lakini kutokana na mlipuko wa corona viongozi hao wa serikali na mataifa saba watazungumza kwa njia ya video.

Viongozi wa ngazi ya juu wa mataifa yaliostawi zaidi kiviwanda duniani ya Uingereza, Canada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Japan na Marekani hukutana mara moja kwa mwaka kujadili masuala muhimu ya kidunia. Mwaka huu, Rais wa Marekani, Donald Trump, ndiye alipaswa kuwa mwenyeji wa mkutano huo. **DW**

## Madaktari wastaafu waombwa kurudi kazini

**LONDON, Uingereza**

UINGEREZA imewaomba madaktari wastaafu kurudi kazini ili kusaidia kukabiliana na janga la Corona huku Waziri Mkuu wa Italia akitoa wito kwa Umoja wa Ulaya kutumia uwezo wake imara wa kifedha kupambana na janga hilo.

Baraza la Wauguzi na Wakunga nchini Uingereza, limewaandikia barua zaidi ya wauguzi 50,000 pamoja na madaktari 15,000 waliostaafu ili kuwaomba kurudi kazini kwa ajili ya kusaidia mapambano hayo.

Kadhalika, wanafunzi wanaosomea taaluma ya matibabu ambao wako mwaka wao wa mwisho, wamepewa nafasi muhimu kutumia ujuzi wao kukabiliana na virusi hivyo.

Kwa sasa idara ya afya nchini Uingereza inaweka wazi vitanda 30,000 kwa kuahirisha opasuaji zisizohitaji dharura na kutoa huduma za kijamii kwa wagonjwa ambao wanakaribia kupata nafuu.

Vilevile, idara hiyo ya afya ilisema inatafuta hospitali binafsi na za kijamii 10,000 ili kukidhi mahitaji ya dharura.

Hatua zote hizo zimechukuliwa kwa ajili ya kushughulikia janga la hivi sasa la Corona.

Ofisa mkuu wa wauguzi nchini humo, Ruth May, alisema: "Hatuwezi kufanikiwa katika hili pekee yetu, ninatoa wito kwa wauguzi wastaafu kutusaidia wakati huu wa mlipuko wa virusi vya Corona kwa sababu nina amini kuwa mnaweza kutusaidia kuokoa maisha"

Nchini Italia, Waziri Mkuu wake, Giuseppe Conte, ameutolea wito Umoja wa Ulaya (EU) kutumia uwezo wao imara wa fedha kupambana na mlipuko wa Corona.

Katika mahojiano na gazeti la Financial Times, Conte ametaka EU ubadilishe utaratibu wake wa kutoa mikopo hasa kwa nchi zenye kutumia sarafu za Euro na ambazo zinakabiliwa na madeni ili kuzisaidia kupambana na corona.

Rais wa Halmashauri Kuu ya EU, Ursula von der Leyen, alisema "Nina habari nzuri kwa Italia. China iko tayari kutuma barakoa milioni mbili. Kati ya hizo, 200,000 ni barakoa maalum.

"Pia viko vifaa vya upimaji elfu 50. Tunatuma zote hizo kama Umoja wa Ulaya kwa sehemu inayohitaji zaidi msaada nayo ni Italia. Vifaa hivyo vikitufikia, tutavituma vyote wiki ijayo nchini Italia."

Nchi hiyo imefunga na kusimamisha shughuli katika bandari zake katika hali ya kuzuia kuenea kwa virusi vya Corona.

Wizara ya uchukuzi imeziagiza meli ambazo tayari ziko baharini kurudi bandarini na watu wote kufanyika vipimo.

**Reuters/AFP**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.
Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

# Mauaji Harusini-5

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Siku isiyo na jina akiwa kijiweni kwake Ilala Bungoni alifika mtu mmoja wa makamu hivi. Alipokelewa na mmoja kati ya marafiki zake. Wakaenda pembeni na kuteta.

Rafiki yake hiyo, Seif, alirudi kwa wenzake na kuwapa mchongo kuwa jamaa alikuwa anahitaji mtu wa kazi na kama kuna mtu anamfahamu, basi ampeleke.

"Kazi gani." Aliuliza Tamim.

"Kazi ngumu, siyo kama hii tunayoifanya. Jamaa anatafuta mtu anayeweza kumuua mtu aliyemdhulumu mali zake." Seif alisema na kuwatazama wenzake waliokuwa kwenye benchi kijiweni hapo.

"Jamaa kadhulumiwa mzigo, sasa jamaa kila anapofuatilia anamzingua, halafu kwa siku za karibuni akaanza kumtishia maisha. Sasa kaona bora yeye amuwahi kabisa. Kama kuna mtu anamfahamu anayeweza kuifanya kazi hiyo ampeleke na yeye atapata cha juu."

"Mwambie aje tuelewane, hiyo kazi mimi naweza kuifanya." Tamim alijibu kwa kujiamini na kusababisha mshangao na mshtuko kwa pamoja kwa wenzake.

Wanachojua ni kwamba Tamim na wao ni matapeli, wanaopata pesa kwa kudanganya watu na si kukaba, au kuua, inakuwaje leo mwenzao aonyeshe kuwa anaweza kazi hiyo, ili mradi tu anayetaka kufanyiwa kazi hiyo awe na bastola?


Ni shilingi milioni mbili tu ndizo zilizomuingiza Tamim kwenye dili hilo, huku rafiki yake Seif alilamba shilingi laki mbili kwa ajili ya kuendesha bodaboda tu.

Alichotaka ni kupewa picha ya anayehitajika kufa, lakini pia mawasiliano kuwa yuko wapi.

Siku ya tukio, simu ilipigwa na kuambiwa kuwa yupo kwenye gari aina ya noah, ilitoka Ilala kwenda Buguruni.

Kwa sababu wao wenyewe walikuwa Ilala hawakuna na papara. Walikaa tayari na wakaliaona gari hilo likipita. Wakaliunganishia kwa nyuma, Seif akiendesha na Tamim kuwa nyuma kama abiria hivi. Hakuna yoyote aliyekuwa akijua nini kinaendelea zaidi yao tu.

Seif aliambiwa aendeshe bodaboda hadi awe pembeni ya gari lile. Gari lilipokuwa sambamba na pikipiki, Tamim aliona ndani ya gari kulikuwa na watu watano pamoja na dereva, hivyo ilikuwa ni vigumu kujua mlengwa ni yupi pamoja na kuwa ana picha yake. Alichofanya akaita jina lililopo kwenye picha ya mlenngwa 'Ally?" Aliita.




Mwenye jina hilo alitoa kichwa dirishani. Alikuwa katikati ya siti ya nyuma. "Wapite kwa kasi." Tamim alimwambia Seif. Waliokuwa kwenye gari walishangaa mtu kumwita mwenzao, lakini hakumwambia kitu. Hata hivyo na wao walipotezea.

Bodaboda lilikata mtaa mmoja kuiruhusu gari ipite. Seif na Tamim walirejea tena kwenye barabara kuu baada ya gari kupita. Ilikuwa kama kona ya Barabara ya Mandela na Uhuru, ameneo ya Buguruni Mataa. Mita kama hamsini hivi, Tamim alichomoa bastola na kulenga kwenye kioo cha nyuma sehemu ya katikati, akaachia risasi mbili zilizotoboa kioo na kuzusha taharuki eneo hilo. "Geuza Bodaboda turudi." Alimwambia Seif. Saa chake baadaye habari zikaja kuwa Ally amefariki baada ya kupigwa risasi na watu wasiojulikana.

Kazi hiyo ilimpa heshima kubwa kwa wahalifu, hasa shabaha yake. Akapata tenda zaidi na zaidi. Hivyo ndivyo alivyoingia kwenye kazi hiyo na kupata tenda ya kuua maharusi Grace na Patiyo.

***************************************

Sauti za vilegele zilisikika nje ya Kanisa na Mtakatifu Joseph jijini Dar es Salaam. Ilikuwa ni baada ya ndoa kufungwa kati ya Grace na Patiyo ambaye ni mfanyabiashara maarufu nchini.

Nyimbo za dini zilikuwa zikiimbwa na ustadi, maharusi wakiwa wameshikana mikono kuelekea kwenye gari aina ya Ranger Rover la kisasa lililokuwa limepambwa, likapambika.

Kulikuwa na magari zaidi ya 70 yaliyokuwa kwenye msafara huo ambao ulikuwa ukitoka eneo la Kanisa, kuelekea Kibada, maeneo ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Kwa sababu ilikuwa ni harusi, na zilihitajika mbwembwe za aina yake, kiongozi wa msafara, au mkuu wa itifaki, aliamuru msafara wa maharusi usiende Feri kwenye kivuko kwa sababu wahudhuriaji wa wasindikizaji wasingepata muda wa kujimwayamwaya, badala yake wangetumia muda mwingi kusubiri pantoni, badala yake aliutaka ukate kulia kuelekea maeneo ya Kurasini wakapite daraja jipya, kabla ya kuingia Kigamboni.

Hii ingewapa fursa watu waliokuwa ndani ya magari kufurahi, kuimba na kucheza kwa muda mrefu wakati wakielekea nyumbani kwa bwana harusi.

Tayari kwenye magari binfasi na mabasi yaliyokodiwa kwenda na kurudi kutoka Kanisani, watu walishaachа kuimba nyimbo za Kanisani, sasa ikawa zamu ya nyimbo wanazozijua wenyewe.

Kuna waliomba nyimbo za taarabu. Wengine wakaimba nyimbo za kwaya. Wapo waliomba nyimbo za makabila mawili ya bwana na bi harusi. Walioimba nyimbo za bongo fleva wapo. Singeli ndiyo usiseme. Ili mradi tu kila ndugu, jamaa na marafiki walioalikwa kwenye sherehe hiyo walijimwayamwaya walivyotaka.

Ilikuwa ni burudani ya aina yake kila wanapopita. Wananchi waliokuwa pembeni walikuwa wakishuhudia msafara mrefu, wenye magari kadhaa ya kifahari, lakini mabasi makubwa na madogo yaliyokuwa na wamesheheni watu waliokuwa wakiimba kwa bidii na mbwembwe za aina yake, kusherehekea harusi hiyo.

*********************************

Fadhili Kidaga alikuwa ametulia tuli kwenye siti ya mbele kushoto, ndani ya gari ndogo iliyokuwa ya 15 kutoka ilipokuwa iliyochukua maharusi.

Ingawa kazi iliyokuwa mbele yake yeye na wenzake ilikuwa kubwa, lakini hakuonekana na wasiwasi hata kidogo.

Alikuwa na wenzake kwa simu akiwataka wasifanye kosa lolote la kiufundi litalokochelewesha opereheni yao, au kuifanya iharibike kabisa.

Tofiki Seif yeye alikuwa kwenye usukani kama kawaida. Pale yeye mwenyewe alijiona kama hayupo kazini. Kazi ataifanya pale tu tukio la mauaji litakapotokea. Hapo ndipo kila mmoja anamjua kaka yeye ni nani na kumheshimu. Akiwa kwenye msafara wa maharusi alijiona tu kama anafanya mazoezi.

Michael Sabuni, yeye alijipenyeza hadi kwenye gari la wapiga picha mnato na wachukua picha za video.

Kuna kifaa ambacho kiliwaharibikia wachukua video waliopewa tenda hiyo rasmi, lakini yeye kwa uzoefu wa kazi kama hizo alikuwa nacho, hivyo baada ya hapo vijana hao watatu hawakumtenga Michael.

Hata alipowaomba apande kwenye gari yao ambayo yenyewe ipo mbele ya gari la maharusi walikubali, kwani pamoja na kwamba aliwasaidia kufaa hicho, lakini pia alionekana ni mtaalam wa kuchukua picha za video, hivyo kuwaelekeza kupicha picha nzuri zaidi na zitakazowavutia wenyewe.

Awali Michael alijitambulisha kama ni mpiga picha za mnato na video ambaye amelipwa na kaka mdogo wa bwana harusi kwa ajili ya kumbukumbu yake.

Jamaa hao hawakufahamu kuwa alikuwa mmoja kati ya watu waliokuwa kwenye mpango kamambe ya kunyofoa uhai wa watu wale wanaowachukua picha za video.

Tamim Hussein, yeye alikuwa nyuma ya gari mwendesha bodaboda, aliyekuwa kati ya waendesha bodaboda zaidi ya 50 zilizokuwa zimetangulia kwenye msafara huo wa harusi, baadhi yao wakifanya mbwembwe za kufurahisha na za hatari zilizowavutia na kuwashangaza wengi waliokuwa wakikutana na msafara huo.

Hakutaka kupanda gari la Kidaga, mpaka pale atakapotimiza mpango waliopanga, lakini pia ilikuwa ni kuwapoteza maboya watu na askari polisi ambao baadaye wataanza kufuatilia mkasa huo.

***********************************

Ilikuwa ni hatua 50 tu ambazo bwana na bibi harusi walikuwa wamezipiga kuelekea kwenye hema kubwa la kisasa lenye nakshi, lililokuwa nje ya jumba la fahari.

Geti lilikuwa wazi ili kuwawezesha umati wa wahudhuriaji kuingia ndani ya uwanja mkubwa, lakini baadhi ya magari, hasa mabasi mkubwa yakiwa yamebaki nje ya geti, lakini baadhi ya magari madogo yakiwa yameruhusiwa.

Ilikuwa ni tafrija ya nyumbani kwa siku hiyo, huku kesho yake kukiwa na sherehe kubwa kwenye hoteli kubwa ya kifahari katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Ghafla sauti kali isiyotarajiwa sehemu kama hiyo ikasikika. Kabla yoyote yule hajajua ni ulikuwa ni mlio wa kitu gani, mlio mwingine unaofanana na ule ukarindima. Hakuna aliyejua nini kimetokea.

Ilikuwa imetimia saa 11:00 jioni. Ni mlio uliosababisha baadhi ya watu kusambaratika huku na huko, kila mmoja kuokoa uhai wake.

Haukuwa mlio wa kawaida. Lakini walichotambua ni kwamba haukuwa mlio wa heri, bali ni wa shari, unaoashiria hatari. Kila mmoja aliyekuwa kwenye sherehe hiyo hakujua anakimbilia wapi au anaelekea wapi. Ilichukua dakika nyingi sana kutambua milio ile miwili ilikuwa ni ya bastola.

**Itanedelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DANIEL NGEMERA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 122 CWL TOYOTA ISUZU.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No: 9910812003087.

115674702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

EDITH KANYENYE MBENA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA MARK11 yenye namba za usajili T 463 AHG. Chassis No.LX800019725, Engine No. 2L2216163.

Yeyote atakaye iona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/500944/2019.

115675102

### CHETI KIMEPOTEA



SCOLASTICA MAZOLEKA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0204/0256 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia JANGWANI SEKONDARI mwaka 1997.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/OST/RB/244361/2020.

### KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

SHABANI IBRAHIM MAKOMBE anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaj iliyokuwa na namba ya usajili MC 194 BYN yenye chasis namba MD2A25BZ9JWL88247 injini namba AZZWJL25397.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: IRI/MUF/RB/178506/2020

156750

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

CRISPIN M. SILAYO anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 468 AMW LANDROVER PICKUP.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: DAR/KIJ/RB/218947/2020.

156753

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

PRISCA SIMON KALLINGA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 214 DPV TOYOTA IST. Chassis namba NCP600235942. Engine namba 2NZ3991353.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No. 9910812117875.

156758

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

RAPHAEL MBUNILE SHITINDI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 236 BZP TOYOTA NOAH. Chassis namba AZR600277789. Engine namba IAZ4781323.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MBE/RUJ/RB/450117/2019.

156757

### KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

WINFRIDA MPAGAMA ALPHANIES anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaj yenye namba za usajili MC 860 CLD.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MBE/MBE/RB/83230/2020.

156756

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ANNA MARCO NGONGI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISH CANTER YENYE NAMBA ZA USAJILI T554DGZ. YENYE CHASSIS NO FE51CB569352 NA ENGINE NO 4D33J00154.

KWAYOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI KAH/ / TR /RB/ 115/2020

115675902

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ALMALI A. MSANGI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 393 AWR NISSAN TIPPER.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: DAR/KIJ/RB/218934/2020.

156754

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY
IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA

CIVIL APPEAL No 21/2019
(Arising from civil case Application no 27/2018 at Bukoba District Court and Civil Appeal 2/2018 of Bukoba urban Primary Court)

DORICE EVODIUS ........................APPLICANT
VERSUS
LUCIA KATO .....................RESPONDENTS

TO, LUCIA KATO

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Civil Appeal No. 21 of 2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 23th day of April, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge L. G. Kairo. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 19th day of March, 2020.

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

156749

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO

**Usimamizi wa mirathi No;83/2020**

Ombi la MOHAMED HAMISI MWAMPEPO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMISI SELEMANI MTALISU

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 20/03/2020.

1156761

JAMUHURI YANMUUNGANI WA TANZANIA
MAHAKAMA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO NGOREME
WILAYA YA SERENGETI.
KUITWA SHAURINI: (Mdaiwa)
SHAURI LA MADAI/NA 16-2020

Kwa: MARWA SESE KYAMBIRYA
WA KIJIJI CHA WEGERO.

Unajulishwa kufika Mahakamani mnamo tarehe 26 mwezi March 2020 muda wa saa 2:00 asubuhi mbele ya Mh. Hakimu ili kujibu Madai madai ya fidia jumla ya TSHS:5,754,430/=za deni.

Fika bila kukosa mara upatapo wito huu.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 19 mwezi march 2020.

Hakimu Mkazi
Mahakama ya Mwanzo Ngoreme

115676202

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
YAH: SHAURI NAMBA 25 LA 2019
NASIR MAKATA MWINYIMTWANA.........MDAI
DHIDI YA
SEIF MWALIMU ALI NA WENZAKE 10....................WADAIWA

KWA: RAJABU SHEHE – POPOTE ULIPO

NASIR MAKATA MWINYIMTWANA,
amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 15/4/2020 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 15/3/2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
TANGA

156765


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SKRINIAR:

## FERNANDES NDIO MCHEZAJI WANGU BORA

**MILAN, Italia**

BEKI wa Inter Milan, Milan Skriniar, amemuelezea nyota wa Manchester United, Bruno Fernandes, kama mmoja wa mchezaji mwenzake bora zaidi.

Skriniar na Fernandes walitumia pamoja mwaka mmoja kwenye soka la Italia katika Klabu ya Sampdoria kabla ya kila mmoja kwenda upande wake.

Miamba wa Serie A, Inter wakafanikiwa kumsajili Skriniar kutua kwenye jiji la Milan mwaka 2017, huku Fernandes akienda kujiunga na Sporting CP kabla ya kutua kwa miamba wa Ligi Kuu England, United Januari mwaka huu.

Fernandes amekuwa na mwanzo mzuri pale Old Trafford na Skriniar amemsifia kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno.

"Nafikiri Bruno Fernandes ni mmoja wa mchezaji mwenzangu bora zaidi kuwahi kucheza nae," alisema Skriniar wakati wa mahojiano ya maswali na majibu kwenye tovuti ya Inter.

"Mara zote nilikuwa napenda kucheza nae na nilifurahia sana

# NYOTA WA ZAMANI WA ARSENAL WAFUKUZWA KLABUNI

**GENEVA, Uswisi**

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Johan Djourou na Alex Song ni miongoni mwa wachezaji tisa waliofukuzwa na klabu ya Uswisi ya Sion kwa kukataa kupunguziwa mishahara yao wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona

Ligi kuu ya nchi hiyo imesimamishwa kutokana na mlipuko huo na hivyo klabu kujikuta haina vyanzo vingine vya kuingiza mapato na kuamua kupunguza mishahara ya wachezaji.

Kwa mujibu wa ripoti ya gazeti la The SDA na televisheni ya RSI, wachezaji waliotemwa nni pamoja na nahodha, Xavier Kouassi, Pajtim Kasami, Ermir Lenjani, Seydou Doumbia, Mickael Facchinetti, Christian Zock na Birama Ndoye.

Imeripotiwa kwamba wachezaji hao walikataa kusaini makubaliano ya kupunguziwa mishahara yao kwa kipindi hiki ambacho ligi imesimama.

Ligi ya nchini Uswisi ilisimamishwa Machi Mosi mwaka huu pamoja na kupiga marufuku ya mikusanyiko yoyote yenye watu zaidi ya 1,000.

Sion ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu Uswisi, Super League, yenye timu 10.

# Rakitic sasa rasmi kwenda Sevilla

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA wamekubali kumpoteza Ivan Rakitic na inaeleweka kwamba anataka kwenda kumalizia soka lake Sevilla, kwa mujibu wa magazeti ya Hispania.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatian alijiunga na Barca mwaka 2014 baada ya misimu mitatu na nusu ya mafanikio pale Seville, na imeripotiwa kwamba anataka kurudi kule kipindi cha majira ya joto.

Ripoti ya magazeti ya Hispania imebainisha kwamba, Barcelona wanajua huu ni msimu wao wa mwisho kuwa na Rakitic, wakati akijinadaa kurudi kwenye uwanja wa Sanchez-Pizjuan kuanzia msimu wa 2020-21.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alikataa nafasi ya kujiunga na Juventus Januari, huku vyombo vya habari vya Hispania vikiripoti kwamba miamba hao wa Italia walitoa ofa ya pauni milioni 39 kwa ajili ya kupata huduma yake.

Rakitic mwenyewe ameonesha nia ya kutaka kurudi Seville ikiwa ni miaka sita baada ya kuondoka, na atalazimisha uhamisho wake kipindi cha majira ya joto licha ya mkataba wake wa sasa kumalizika Juni 2021.

Huko ndio alikokutana na mke wake, na alishinda taji la Ligi ya Europa kwenye msimu wake wa mwisho kabla ya kujiunga na Barcelona.

## HABARI MICHEZO



# POCHETTINO

## ATAMANI KURUDI KUINOA TIMU YAKE YA UTOTO

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino ana matumaini siku moja atarudi kuinoa timu ya Newell's Old Boys, pamoja na nyota wa Barcelona, Lionel Messi kwenda kumalizia soka lake pale.

Pochettino alianza maisha yake ya uchezaji pale Newell's katika kikosi cha vijana mwaka 1989 kabla ya kujiunga na miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Espanyol mwaka 1994.

Majaliwa ya Pochettino bado hayajajulikana baada ya kufukuzwa pale Tottenham Novemba mwaka jana - huku akihusishwa na timu kama Manchester United na Real Madrid.

Na sasa Pochettino, amebainisha nia yake ya kutaka kurudi Newell's pamoja na mshindi mara sita wa Ballon d'Or, Messi - ambaye naye alicheza pale akiwa kijana mdogo.

"Natumaini kurudi kwenye klabu ile siku moja," amesema Pochettino mwenye umri wa miaka 48 akiiambia redio del Plata.

"Naweza kusubiri, itafaa kama itakuwa ndani ya miaka 10, nikiwa na (Lionel) Messi."

# Lukaku: Nilikaribia kujiunga Juventus

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku "alikaribia " kujiunga na Juventus mwaka jana, lakini nafasi ya kuwa chini ya Antonio Conte ndio kulikomfanya abadili uamuzi na kusaini Inter Milan.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alimaliza kipindi chake cha misimu miwili pale Manchester United kwa kujiunga na Inter kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni euro milioni 80 Agosti 2019.


Lukaku amekuwa na mwanzo mzuri kwenye soka la Italia, akifunga mabao 23 katika mechi 35 alizocheza kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 amebainisha alikaribia kujiunga na Juve ambao ni wapinzani wa Inter.

"Kwa uhakika kabisa nilikaribia kujiunga na Juve, lakini akili yangu ilivutiwa na Inter pamoja na kocha wake," alisema Lukaku katika mahojiano ya televisheni ya mtandao inayomilikiwa na Ian Wright.

"Nikiwa mdogo niliwashabikia sana Adriano, Ronaldo na (Christian) Vieri.

"Kwa uhakika kabisa baada ya Inter kuja na Conte ambaye alinitaka wakati akiwa Chelsea na Juve niliamua kumfuata ili nijionee mwenyewe nini alichonacho."



# Ronaldo, Ramos walinitaka niende Madrid – Lewandowski

**MUNICH, Ujerumani**

CRISTIANO Ronaldo na Sergio Ramos walijaribu kumshawishi Robert Lewandowski kujiunga na Real Madrid miaka mitatu iliyopita, mshambuliaji huyo wa Bayern Munich amedai.

Lewandowski mara kadhaa alikuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakati akiwa anacheza katika klabu ya Borussia Dortmund na baadaye Bayern.

Licha ya jitihada za Ronaldo na Ramos, mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland hivi karibuni alitupilia mbali uwezekano wa kujiunga na Madrid na alisema ana furaha kucheza pale kwenye dimba la Allianz Arena.

Alipoulizwa kama ni kweli kwamba, nahodha wa Madrid, Ramos na mshambuliaji wa zamani Ronaldo walijaribu kumshawishi asaini kwenye klabu hiyo baada ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2017, Lewandowski alijibu: "Ndio!"

Akielezea sababu zilizokuwa nyuma yake kuamua kubakia kule Bundesliga, Lewandowski aliongeza: "Unaweza kwenda kwenye Ligi ya Hispania au katika nchi nyingine, katika klabu kubwa.

"Lakini kwa upande wangu mimi haliku-wa jambo muhimu. Nimeweza kufikia pale nilipokuwa napataka na nataka kuendelea kufanya vizuri.

"Nipo kwenye moja ya klabu bora kabisa duniani, na najua kwamba naweza kuwa na furaha hapa."

Lewandowski amefunga mabao 39 msimu huu, 25 kutoka kwenye Ligi, na amesisitiza hajapoteza njaa ya kuendelea kufunga mabao.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAJIANDAA KUMNASA AUBAMEYANG

●●●Yatajwa kutenga pauni milioni 50 ili kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Gabon...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuandaa ofa ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, washikabunduki hao wanaweza kumuuza nyota wao huyo ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2021.

Maofisa wa Arsenal wameripotiwa kwamba wamekubali mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 hatasaini mkataba mpya na Ole Gunnar Solskjaer yupo tayari kutumia mwanya huo.

Aubameyang amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa kikosi hicho cha Mikel Arteta, huku klabu hiyo ikiwa imetupwa nje kwenye michuano ya Ligi ya Europa na kwa sasa inashika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Arsenal waliilipa Borussia Dortmund ada iliyoweka rekodi ya klabu ya pauni milioni 56 na kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon Januari mwaka 2018.

Barcelona na Paris Saint-Germain pia zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kumsajili mshambuliaji huyo na wanaweza kumshawishi kwa sababu wana nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

Manchester United walimchukua Odion Ighalo kwa mkopo kutoka klabu ya nchini China ya Shanghai Greenland Shenhua Januari baada ya kushindwa kumsajili nyota wa Bournemouth, Josh King.

Ighalo amekuwa na mwanzo wa kuvutia katika maisha yake pale Old Trafford lakini haijajulikana atakaa klabuni hapo kwa muda gani.

United bado haijampata mrithi wa muda mrefu wa Romelu Lukaku na imekumbwa na pigo kwa majeruhi ya Marcus Rashford na Anthony Martial msimu huu.

Aubameyang tayari amefunga mabao 20 kwenye mashindano yote kwa msimu wa 2019-2020 baada ya kufunga mabao 31 msimu uliopita.

Mkuu wa soka wa Arsenal, Raul Sanllehi na Mkurugenzi wa Ufundi, Edu walimtaka nahodha huyo kukubali kusaini mkataba wa muda mrefu, lakini Sanllehi na Mkurugenzi Mkuu, Vinai Venkatesham pia wamedokeza wataepuka kurudia hali ya Aaron Ramsey na Jack Wilshere ambapo wote waliondoka wakiwa wachezaji huru.

Mesut Ozil, Bukayo Saka, Shkodran Mustafi na Reiss Nelson pia wote mikataba yao inamalizika mwaka 2021, lakini inaonekana kuna uharaka zaidi wa kumaliza kwanza majaliwa ya Aubameyang.

## KWA UFUPI

**UNITED YAMTAKA COUTINHO**
MANCHESTER United imeanza kujipanga kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho, mwenye umri wa miaka 27, akitokea Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

**POGBA RASMI SOKONI**
MABOSI wa Manchester United wanajipanga kupokea ofa ya pauni milioni 100 ili kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Paul Pogba. Real Madrid na Juventus zimetajwa kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

**SANTAMARIA ANUKIA VILLA**
ASTON Villa imewasilisha tena ofa kwa Angers ili kuwania saini ya kiungo Baptiste Santamaria baada ya klabu hiyo kuwakatalia katika dirisha la usajili la Januari na bado haijafanya uamuzi wa kutuma ofa nyingine mpya ya kumsajili Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 25 katika majira ya joto. ***(ABC Sevilla, in Spanish)***

**AUBAMEYANG ANUKIA CHELSEA**
CHELSEA inasisitiza inahitaji huduma ya straika wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30). ***(90min)***

**ATLETICO KUMFUNGA PARTEY**
ATLETICO Madrid inajiandaa kumwongezea mkataba kiungo wake raia wa Ghana, Thomas Partey (26), ambapo utamalizika ifikapo mwaka 2025 na kuweka dau jipya la kumng'oa klabuni hapo kufikia pauni milioni 92. Tayari kuna tetesi za nyota huyo kutakiwa na Arsenal na Manchester United. ***(Goal)***

**PJANIC KUONDOKA JUVE**
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Bosnia, Miralem Pjanic (29), anajiandaa kuondoka Juventus katika majira ya joto. Manchester City na Chelsea zinawania saini ya nyota huyo. ***(Corriere dello Sport via Sport Witness)***

**WILLIAN- NITAJITUMA ZAIDI**
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Brazil, Willian (31), amesema ataendelea kuitumikia klabu yake hadi mwisho wa msimu ambapo mkataba wake utamalizika, licha ya mambo yanayoendelea kutokuwa mazuri. ***(Star)***

**MAGALHAES ANUKIA EVERTON**
BEKI wa Lille, Mbrazil Gabriel Magalhaes, ambaye ana umri wa miaka 22, ametajwa kuwindwa na Everton katika dirisha la usajili la majira ya joto. ***(Liverpool Echo)***

**GIANLUIGI AKARIBIA PSG**
GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Donnarumma (21), anatarajia kuondoka AC Milan na kujiunga na Paris St-Germain au klabu nyingine inayoshiriki Ligi Kuu England. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**MILAN YAJIPANGA**
INTER Milan imeieleza Barcelona iko tayari kukamilisha usajili wa straika wa Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez (22), kwa kutoa fedha taslimu na si vinginevyo. ***(Sport - in Spanish)***

**ALABA AIKARIBIA BARCA**
BEKI wa Timu ya Taifa ya Austria, David Alaba (27), anajiandaa kuachana na Bayern Munich huku Real Madrid na Barcelona zikionyesha nia ya kunasa saini yake. ***(Sport Bild - in German)***

**CANTONA KUREJEA UNITED**
MANCHESTER United inatarajia kumrejesha klabuni straika wake wa zamani, Eric Cantona (53), katika majukumu ya ubalozi. ***(Mirror)***

# AZAM YATAMBA ITASHIRIKI MASHINDANO YA KIMATAIFA

**Na Saada Akida**

WAKATI timu yake iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Azam FC, umesema bado wana imani watakata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa katika msimu ujao.

Azam ni mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA na ni moja ya timu nane zilizotinga hatua ya robo fainali ya mashindano hayo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema licha ya kuwa katika nafasi ya pili, pia bado wana imani ya kufanya vema kwenye michezo 10 ya Ligi Kuu Bara iliyobakia.

Popat alisema timu yake haijakata tamaa ya kutwaa ubingwa wa Bara kwa sababu wanaamini katika soka lolote linaweza kutokea kwa vinara wa ligi hiyo, Simba yenye pointi 71.

"Mipango yetu ni kushiriki michuano ya kimataifa, hivyo lazima tupambane kutetea Kombe la FA lakini pia tunahitaji kufanya vizuri katika mechi zilizobakia za Ligi Kuu."

"Licha ya kutoa mapumziko wachezaji wetu kila mmoja amepewa majukumu yake ya kufanyia kazi, ili tutakaporejea tuendelee na mapambano kwa ajili ya ligi na pia Kombe la FA ambalo tunahitaji kupambana kufanya vizuri katika hatua ya robo," alisema Popat.

Aliongeza ana imani timu zote zilizoingia katika hatua hiyo na wanajipanga kuhakikisha wanasonga mbele na kutimiza malengo yao ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

"Muda tulionao si rafiki kutokana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona kuleta madhara na kusababisha mambo mengi kusitishwa kwa muda ikiwamo ligi, kwa upande wetu tayari benchi letu la ufundi limejipanga kwa kuwaandalia wachezaji programu maalum ya mazoezi yao binafsi," alisema Popat.

Aliongeza bodi ya ligi ya timu hiyo inatarajia kutumia muda wa mapumziko kujadili mwenendo wa timu yao katika ligi msimu huu pamoja na kuangalia upungufu na baadaye kukutana na benchi la ufundi linaloongozwa na Aristica Cioaba ili kupanga mikakati ya kuelekea msimu ujao.

"Michakato inaendelea ila kama ilivyo utaratibu wetu sisi kocha ndio mwenye kutuambia mchezaji anayemhitaji, kwa hiyo bado hajatupatia nyota anaowahitaji," Popat alisema.

Uongozi wa klabu hiyo ulitangaza kuwarejesha nchini kwao wachezaji wote wa kigeni, sambamba na kuvunja kambi za timu za vijana.



Msanii wa uchekeshaji, Idris Sultan (katikati), akiwa na watuhumiwa wenzake wanaokabiliwa na kesi ya uchochezi wakitoka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana baada ya kupata dhamana. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Mbao yafunguka kinachowamaliza

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ligi Kuu Bara ikiwa imesimama kwa muda ili kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), uongozi wa Mbao FC umesema tatizo linalosababisha kikosi chao kupata matokeo mabaya kwenye ligi hiyo ni suala la ukata.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Mbao FC, Solly Njashi alisema timu hiyo imekuwa na matokeo yasiyofurahisha kutokana na changamoto ya fedha ambayo imewakumba tangu kuanza kwa msimu.

Njashi alisema wachezaji wamekuwa wakijitahidi kujiandaa lakini inapofika wakati wa viongozi kutekeleza mipango, mambo yanakwenda tofauti.

"Tunapambana sana ili kuwa kwenye ubora wetu lakini tatizo ni fedha, gharama za uendeshaji wa timu ni kubwa, kwa sasa hatuna fedha za kutosha, hali hii inatuumiza na inatusumbua," alisema Njashi.

Alieleza fedha za wadhamini wanazopata kutoka Vodacom na Azam TV hazitoshi kuendesha timu, ingawa zinasaidia kupunguka makali ya ukata waliyonayo.

Mbao FC ambayo iko chini ya Kocha Mkuu, Abdulmutik Haji, ipo nafasi ya 19 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa imejikusanyia pointi 22 kibindoni baada ya kushuka uwanjani mara 28.

# Mtibwa Sugar kujipanga upya

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema janga la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona ( COVID 19), limeharibu mipango yake lakini wanalazimika kujipanga upya.

Mtibwa Sugar ililazimika kuondoka Tanga na kurejea Manungu, mkoani Morogoro baada ya mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal Union uliotarajiwa kuchezwa Machi 18, mwaka huu kuahirishwa.

Katwila aliliambia gazeti hili baada ya kurejea Manungu, wachezaji wa timu hiyo wataendelea kufanya mazoezi huku kila mchezaji akitokea nyumbani kwake.

"Tumeungana na serikali kusimamisha kambi, kwa upande wangu timu itakuwa inaendelea na mazoezi kila mchezaji akiwa anatoka nyumbani ili kujiweka sawa kwa ajili ya kujiandaa na michezo ijayo pindi ligi itakapoanza ,"alisema Katwila.

Kocha huyo alisema kusimamishwa kwa ligi hiyo kumeleta changamoto kutokana na kikosi hicho 'kilichozinduka' na kupata ushindi kujiandaa vema kuikabili Coastal Union lakini, sasa watatakiwa kujipanga upya.

"Kwa upande wangu imeniathiri, tayari nilikuwa nimejipanga kwa ajili ya safari ya Tanga, vile vile niliwapa wachezaji wangu maandalizi ya hali ya juu kuelekea mchezo huo, lakini haukuchezwa na sasa hivi ninajipanga upya kusubiri tarehe nyingine," alisema Katwila.

Aliongeza timu yake bado ina 'kibarua kizito' kuhakikisha inapata matokeo chanya katika mechi zilizosalia ili kujiepusha na janga la kushuka daraja.

# TFF yakumbusha wachezaji kujifua

**Na Shufaa Lyimo**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imewataka wachezaji wote wanaoshiriki katika ligi mbalimbali hapa nchini wasibweteke katika kipindi hiki ambacho ligi hizo zimesimama ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa bodi hiyo, Almasi Kasongo alisema hiki ni kipindi cha wachezaji kuendelea kujifua kwa kufanya mazoezi binafsi ambayo yatawaimarisha na kuwaweka tayari kupambana mara ligi hiyo itakapoendelea.

Kasongo alisema mchezaji anapoacha kufanya mazoezi katika kipindi cha siku 30, anakuwa amejirudisha nyuma na mwili hautakuwa sawa tofauti mwenzake ambaye alikuwa akiendelea kujinoa.

"Katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu imesimama ni vema wachezaji wautumie vizuri muda huu kwa kufanya mazoezi yao binafsi, wakiendelea kusubiri siku mpya ya kuanza ligi endapo janga hili litapungua katika nchi yetu," alisema Kasongo.

Kiongozi huyo alisema endapo ligi hiyo itaruhusiwa kuendelea, viongozi watahakikisha kila mchezaji anakuwa katika hali nzuri kiafya ili kujikinga na maambukizi mapya na amewataka Watanzania kufanya ibada ili janga hili lipite na shughuli nyingine ikiwamo soka ziendelee kama kawaida.

"Ninaomba Watanzania wenzangu tuungane kwa pamoja kuliombea Taifa letu liepukwe na janga la ugonjwa huu wa corona ili taratibu zetu za mpira ziendelee kama kawaida, binafsi jambo hili limenistua kwa kiasi kikubwa,"alisema Kasongo.

Aliwataka wadau wote wa soka nchini kuwa wavumilivu na kusubiri mwongozo mpya wa tarehe ya kuendelea kwa ligi zote za hapa nchini baada ya kupata maelekezo kutoka serikalini kuhusiana na tathmini ya ugonjwa huo wa corona.

# Michezo

Jumamosi Machi 21, 2020

Nipashe




## United yajiandaa kumnasa Aubameyang

HABARI UK 30

# USAJILI YANGA GUMZO JIPYA

## Mbelgiji kukabidhi ripoti kamili ya kiufundi kuhusu hatima ya nyota anaowahitaji na watakaotemwa...

**Na Saada Akida**

MAPEMA! Yanga inatarajia kuanza haraka mikakati ya kukisuka upya kikosi chake kwa ajili ya kufanya vema kwenye msimu ujao baada ya leo kujiandaa ripoti ya kiufundi kutoka kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo Mbelgiji Luc Eymael, imeelezwa.

Ripoti hiyo inatarajiwa kuweka wazi majina ya wachezaji ambao anahitaji kuendelea nao katika msimu mpya na wale ambao 'safari' ya kuitumikia Yanga itakuwa imeishia msimu huu.

Wakati mchakato huo unafanyika, taarifa kutoka Yanga zinasema kuna nyota saba ambao mikataba yao inakaribia kuisha ni pamoja na Said Makapu, Deus Kaseke, Mrisho Ngasa, Juma Abdul, Kelvin Yondani, Jaffary Mohamed na Vincent Andrew.

Hata hivyo, bado mabosi wa Yanga wamekuwa wakiumiza 'kichwa' namna ya kuhakikisha mikataba ya wachezaji wao wa kigeni inaendelea kudumu kutokana na kuwapo kwa taarifa za madai ya fedha za usajili zilizobakia.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredirick Mwakalebela alisema uongozi wa klabu hiyo unatarajia kupokea mapendekezo ya wachezaji wanaotakiwa kuongezwa mkataba na wapya kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

Mwakalebela alisema jukumu la kumpa madaraka Eymael kusimamia mchakato wa usajili lilifikiwa katika kikao cha viongozi wa klabu hiyo ambao wanaamini kocha huyo atalifanya kwa weledi zaidi.

**"Hadi sasa hatujaanza mchakato wowote kuhusiana na wachezaji wa kigeni ambao wanatajwa, Eymael atakabidhi ripoti ya usajili kesho (leo), Kamati ya usajili itapokea mapendekezo ya kocha na kushirikiana katika usajili ikiwamo kuwaongezea mikataba wachezaji anaowahitaji ambao mikataba yao inakaribia kumalizika," alisema Mwakalebela.**

Kiongozi huyo alisema wamejipanga kuhakikisha usajili utakaofanywa na klabu yao utakuwa makini na hatimaye kufikia malengo watakayojiwekea katika msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, Kombe la FA na mashindano mengine watakayoshiriki.

Alieleza Eymael amekuwa akifanya kazi kwa ukaribu na wachezaji mbalimbali huku alipotoka, hivyo Kamati ya Usajili ya Yanga haina mpango wa kumwingilia kwenye maamuzi atakayofanya ili kutekeleza majukumu yake.

"Baada ya kocha kukabidhi ripoti na kutoa mapendekezo ya usajili, kuanzia hapo atasafiri kwenda katika mapumziko mafupi, ratiba ambayo imekuja kufuatia ligi kusimama," alisema Mwakalebela.

Mbali na kocha, klabu hiyo imeandaa utaratibu maalum wa kuwasafirisha wachezaji wake wa kigeni kurejea kwao katika kipindi hiki ambacho ligi imesimama kupisha mapambano ya virusi vya ugonjwa wa corona ambao unasumbua dunia.



Mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Neymar, akifanya mazoezi ili kulinda kiwango chake katika kipindi hiki ambacho ligi mbalimbali duniani zimesimama kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19)kwenye uwanja wa mchezo wa mpira wa wavu jana. **PICHA: MTANDAO**

# Mkude: Hakuna zaidi ya Simba

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kiungo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Jonas Mkude, akisisitiza hakuwahi kusema hana mpango wa kuitumikia Timu ya Taifa (Taifa Stars), ameweka wazi mapenzi yake makubwa aliyonayo kwa Wekundu wa Msimbazi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkude alisema uamuzi wake wa kuitumikia Simba kwa muda mrefu unatokana zaidi na mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo kwa vinara hao wa Ligi Kuu Bara ambao wana pointi 71 baada ya kucheza mechi 28.

Mkude alisema anaumizwa na taarifa ambazo si za kweli zinazungumzwa dhidi yake na mbali na yeye binafsi, hali hiyo humuumiza pia mama yake mzazi.

"Kila mchezaji anatamani kuchezea Timu ya Taifa, kwa hiyo mimi nitakuwa mtu wa ajabu kuikataa Timu ya Taifa, sijawahi kusema kokote kwamba siitaki Timu ya Taifa," alisema Mkude.

Kiungo huyo alikanusha taarifa za 'kujivunja' na kujitoa katika kikosi cha Taifa Stars kilichokuwa chini ya Mnigeria Emmanuel Amunike na alikubaliana na uamuzi wa kuachwa na kocha huyo ambaye mwaka jana alifanikiwa kuipeleka Tanzania kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2019).

Alisema pia bado anahitaji kutoa mchango wake kwa taifa endapo ataitwa lakini akikataa kuzungumzia taarifa za klabu nyingine iwe ya ndani au nje ya Tanzania kwa sababu bado ana mkataba na Simba.

Aliongeza amekuwa akiheshimu ratiba ya mazoezi na amekiri kufanya starehe mbalimbali pale muda wa kufanya hivyo unapomruhusu na hilo hufanywa na watu wengi na si yeye pekee.

"Hakuna mkamilifu, kila binadamu ana upungufu wake, kwa hiyo hata mimi nina upungufu wangu ninakubali,... napenda kucheza zaidi kama kiungo mkabaji, lakini nawakumbusha huwezi kucheza Simba miaka 10 kama huna lolote au huna nidhamu kabisa na bado ukavumiliwa," Mkude alisema.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042